ATHARI YA LUGHA YA KIHA KATIKA UJIFUNZAJI WA LUGHA YA KISWAHILI KATIKA SHULE ZA MSINGI NA SEKONDARI WILAYANI KASULU

RUKIA MSAGO JUMA

TASNIFU ILIYOWASILISHWA IKIWA NI SEHEMU YA KUTIMIZA MASHARTI YA KUTUNUKIWA SHAHADA YA UZAMILI KATIKA LUGHA YA KISWAHILI

IDARA YA ISIMU NA TAALUMA ZA FASIHI YA CHUO KIKUU HURIA CHA TANZANIA

2025

UTHIBITISHO

Aliyeweka sahihi hapa chini amethibitisha kuwa Tasnifu yenye maada "Athari ya Lugha ya Kiha katika ujifunzaji wa Lugha ya Kiswahili" katika Shule za Msingi za Sekondari Wilayani Kasulu anapendekeza ikubaliwe na Chuo Kikuu Huria cha Tanzania kwa ajili ya kutimiza takwimu zitakazopelekea kufanya utafiti huu.

…………………………………….

Dkt. Albert Z. Memba

…………………………………

Tarehe

HAKIMILIKI

Sehemu yoyote ya Tasnifu hii hairuhusiwi kukaririwa wala kunakiriwa kwa njia yoyote ya Kielektroniki wala kunakiri pasipo kupata idhini ya mandishi kutoka kwa mwandishi wa pendekezo hili la utafiti bali kufuata sheria.

TAMKO

Mimi, Rukia Msago Juma, natamka na kuthibitisha kwamba Tasnifu iitwayo “Athari Ya Lugha Ya Kiha Katika Ujifunzaji Wa Lugha Ya Kiswahili katika Shule za Msingi na Sekondari Wilayani Kasulu ni kazi yangu mwenyewe na halijawai kuwasilishwa popote pale kwa lengo la kukusanyia Takwimu za utafiti wangu.

………………………………..

Saini

……………………………….

Tarehe

TABARUKU

Tasnifu hii naitabarukia kwa wazazi wangu **Msago** na **Ziana** na kwa wanafunzi wote wa Kiswahili Isimu na Fasihi Chuo Kikuu cha Tanzania na kwa wale wote wanaosoma Kiswahili.

SHUKRANI

Awali ya yote, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunisaidia kufanikisha kazi yangu hii. Kufanikiwa kwa utafiti huu wa “athari ya lugha ya Kiha katika ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili katika Shule za Msingi na Sekondari Wilayani Kasulu imetokana na misaada ya watu mbalimbali.

Shukrani za dhati zimfikie msimamizi wangu mkuu Dkt Albert Memba kwa juhudi zake zote za kunisimamia na kunisahihisha mpaka kufikia kiwango hiki. Vile vile namshukuru kwa kunipa moyo uliyonifanya nifanye kazi hii. Napenda kuwashukuru wataalamu wa Lugha ya Kiswahili kwa ujumla kwa ushirikiano mzuri walioutoa kwangu mpaka kufanikisha kazi hii.

Pia shukrani zangu maalum ziende kwa Walimu wote walionifundisha Isimu ya Lugha katika Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania Kituo cha Mbeya.

IKISIRI

Tasnifu hii ina lengo la kuona athari ya lugha ya Kiha katika ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili katika shule za msingi na sekondari wilayani Kasulu. Utafiti huu una malengo mbalimbali. lengo kuu ni kuchunguza athari ya Kiha katika ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili. Pia, malengo mahususi ni kuainisha athari hasi na chanya za lugha ya Kiha, pili, kuainisha sababu mbalimbali za lugha ya Kiha kuathirhi ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili pamoja na kutafuta njia za kutatua athari zinazopelekea lugha ya Kiha kuathiri lugha ya Kiswahili. Utafiti huu umetumia nadharia ya mawasiliano. Nadharia hii ina lengo la kukuza na kuweka mikakati mizuri kwa wale wanaojifunza lugha ya pili.

Utafiti huu umefanyika katika mkoa wa Kigoma, taasisi mbili, shule za msingi na shule za sekondari, wakiwemo walimu na wanafunzi na wanakijiji wa kijiji cha Lusesa. Utafiti huu utatumia mbinu za utafiti ambazo ni hojaji, mahojiano na majadiliano ya makundi katika kukusanya takwimu. Utafiti lina jumla ya watafitiwa 45 miongoni mwao wakiwa walimu 10, wanafunzi wa sekondari 10, wanafuzi wa msingi 10 na wanajamii 15 ambao watatusaidia kukusanya takwimu, mapendekezo ya mtafiti ni kwamba lugha ya Kiha inaleta athari kwa watu wa lugha Kiha wanapokuwa wanajifunza lugha ya Kiswahili sanifu. Hivyo, ipo haja ya kuanza kujifunza lugha ya Kiswaili mazingira yote.

YALIYOMO

UTHIBITISHO .... **ii**

HAKIMILIKI .... **iii**

TAMKO .... **iv**

TABARUKU .... **v**

SHUKRANI... **vi**

IKISIRI .... **vii**

YALIYOMO .... **viii**

ORODHA YA MAJEDWALI .... **xiv**

SURA YA KWANZA.. **1**

UTANGULIZI WA JUMLA **1**

1.1 Mada ya Utafiti... 1

1.1.1 Lugha ya Kiha 1

1.1.2 Lugha ya Kiswahili... 2

1.1.3 Muingiliano baina ya Lugha Mbili Tofauti 2

1.2 Usuli wa Tatizo 3

1.3 Tatizo la Utafiti 4

1.4 Malengo ya Utafiti... 5

1.4.1 Lengo Kuu... 5

1.4.2 Malengo Mahususi 5
1.5 Maswali ya Utafiti 5
1.6 Umuhimu wa Utafiti 5
1.7 Mawanda na Mipaka ya Utafiti 6
1.8 Mpangilio wa Tasnifu / Muundo 7
SURA YA PILI 8
MAPITIO YA KAZI TANGULIZI 8
2.1 Utangulizi 8
2.2 Mapitio ya Kazi Tangulizi 8
2.3 Maana ya Istilahi Zilizotumika Kwenye Utafiti 12
2.3.1 Lugha 12
2.3.2 Lugha Asili 12
2.3.3 Lugha Ya Pili 13
2.3.4 Ujifunzaji Lugha 13
2.4 Pengo la Utafiti 13
2.5 Kihunzi cha Nadharia 14
2.6 Nadharia ya Mawasiliano 14
2.7 Mfumo wa Dhana 15
2.7.1 Tofauti ya Kujitegemea 16
2.7.2 Tofauti Tegemezi 16

2.8 Hitimisho....16

SURA YA TATU....18

MBINU ZA UTAFITI....18

3.1 Utangulizi....18

3.2 Mkabala wa Utafiti....18

3.2.1 Mkabala wa Kimaelezo....18

3.2.2 Mkabala wa Kitakwimu....18

3.2.3 Mkabala wa Mchanganyiko....18

3.3 Eneo la Utafiti....19

3.4 Uteuzi wa Walengwa....19

3.4.1 Sampuli na Usampulishaji....20

3.5 Vyanzo vya Data....21

3.5.1 Data za Msingi au Awali....21

3.5.2 Data za Upili....21

3.6 Ukusanyaji wa Data....21

3.6.1 Vifaa vya Kukusanyia Data....22

3.6.2 Mbinu za Ukusanyaji data....22

3.6.2.1 Mahojiano au Usaili....23

3.6.2.2 Hojaji....24

3.6.2.3 Majadiliano....24

3.7 Uhalali na Uthibiti wa Matokeo ya Utafiti 25
3.7.1 Maadili ya Utafiti 25
3.7.2 Uthabiti 25
3.8 Hitimisho..26
SURA YA NNE 27
UWASILISHAJI, UCHAMBUZI NA MJADALA WA DATA ZA UTAFITI ...27
4.1 Utangulizi...27
4.2 Majibu ya Maswali ya Utafiti 27
4.2.1 Athari ya Lugha ya Kiha Katika Ujifunzaji wa Lugha ya Kiswahili 27
4.2.2 Kuongezeka kwa Baadhi ya Viambishi Visivyohusika.............................28
4.2.3 Uelewa Mdogo wa Wanafunzi Wakati wa Ufundishwaji 30
4.2.4 Athari katika (Sauti) / Fonolojia...31
4.2.4.1 Kushindwa Kutamka Baadhi ya Sauti (Ubadilishaji wa Fonimu) 31
4.2.4.1.1 Sauti /l/ Kutamkwa Kama Ssauti /r/ 32
4.2.4.1.2 Sauti/g/ Kutamkwa kama sauti /k/..32
4.2.4.1.3 Sauti /dha/ kutamka kama Sauti /za/.......................................33
4.2.5 Athari ya Kimsamiati...34
4.2.6 Athari ya Kimuundo 34
4.2.7 Athari ya Kimaana...35

4.3 Sababu Zinazopelekea Lugha ya Kiha Kuathiri Ujifunzaji wa Lugha ya Kiswahili 38

4.3.1 Athari ya Lugha Mama 38

4.3.1.1 Kuthamini Lugha Mama Zaidi Kuliko Lugha Nyingine 39

4.3.1.2 Ukosefu wa Baadhi ya Sauti Katika Lugha ya Kiha 40

4.3.1.3 Malezi 41

4.3.1.4 Kusahau Baadhi ya Msamiati ya Lugha ya Kiswahili.............................42

4.3.2 Mwingiliano Mdogo wa Makabila Tofauti..43

4.4 Ni Njia Zipi Zitumike Kuondoa Athari ya Lugha ya Kiha Katika Ujifunzaji wa Lugha Ya Kiswahili 44

4.4.1 Kuwafundisha Lugha ya Kiswahili Wakiwa Bado na Umri Mdogo..........44

4.4.2 Kuhimiza Kuongea Lugha ya Kiswahili Wawapo Nyumbani...................45

4.4.3 Ufundishaji wa Kiswahili Sanifu Mashuleni 46

4.4.4 Kiswahili Kuwa Lugha Rasmi ya Kufundishia Elimu ya Sekondari 47

4.4.5 Matumizi ya Kamusi ya Kiswahili 47

4.4.6 Kiswahili Kitumike Katika Shughuli Za Kijamii Zinazotakiwa Kutumia Lugha ya Kiswahili...48

4.4.7 Kufanya Semina na Mijadala Mbalimbali ya Lugha ya Kiswahili 49

4.4.8 Kutoa Elimu Kuhusu Lugha ya Kiswahili 49

4.4.9 Kutoa Adhabu Kwa Wanafunzi Wanaoongea Lugha Tofautitofauti Na Lugha Ya Kiswahili Wawapo Shuleni 50

SURA YA TANO 52

MUHTASARI, MAPENDEKEZO NA HITIMISHO...52

5.1 Utangulizi...52

5.2 Muhtasari wa Utafiti Huu 52

5.3 Matokeo ya Utafiti..53

5.2.2 Kubainisha sababu za Lugha ya Kiha kuathiri Lugha ya Kiswahili katika Ujifunzaji katika Shule za Msingi na Sekondari.......................................54

5.2.3 Kubaini njia za kutumia ili kupunguza athari za Lugha ya Kiha katika Ujifunzaji wa Lugha ya Kiswahili katika Shule za Msingi na Sekondari 54

5.3 Mchango wa Utafiti...55

5.4 Mapendekezo ya Utafiti...55

5.5 Mapendekezo ya Tafiti zijazo 56

5.6 Hitimisho...56

MAREJEREO...58

ORODHA YA MAJEDWALI

Jedwali Na. 3.1: Mchanganuo wa Watafutwa 21

Jedwali 4.1: Kuongezeka kwa Baadhi ya Viambishi Visivyohusika.........................29

Jedwali Na. 4.2: Idadi ya Watafitiwa Kutomuelewa Mwalimu Wakati wa Kufundishwa Kutokana na Athari ya Kiha 31

Jedwali Na. 4.3:. Sauti /r/ kutamkwa kama Sauti /l/ 32

Jedwali Na. 4.4: Sauti /g/ Kutamkwa Kama Sauti /k/ 33

Jedwali Na. 4.5: sauti /dh/ kutamkwa kama sauti /z/...33

Jedwali Na. 4.6: mifano ya athari za kimsamiati 1 34

Jedwali Na. 4.7: Sentensi za Kiha zinavyoathri muundo wa Sentensi za Kiswahili ..35

Jedwali Na. 4.8: Linaonesha Mfumo wa Athari za Kimaana / Semantiki 35

Jedwali Na. 4.9: Mfano wa Viambishi vya Njeo Katika Maneno ya Kha 37

Jedwali Na. 4.10: Viambishi Tamati 38

Jedwali Na. 4.11: Maneno ya Kiswahili Yenye Sauti /l/ na Kutamkwa Kama Sauti /r/ 41

Jedwali Na. 4.12: Katika Lugha ya Kiha Hawana Sauti /k/ na Badala yake Kuweka Sauti /g/ Kwa Kuwa tu Katika Lugha yao Hawana Sauti /k 41

SURA YA KWANZA

UTANGULIZI WA JUMLA

1.1 Mada ya Utafiti

Utafiti huu unahusu athari ya lugha ya kiha katika ufunzaji wa lugha ya Kiswahili wilayani kasulu katika shule za msingi na secondary: utafiti huu ulishughulikia athari zote yaani athari chanya na hasi katika Nyanja zote yaani kifonolojia , mofonolojia, sintasksia na kisemantiki katika sura hii ya kwanza vipo vipengele mbalimbali vilivyozungumziwa ndani yake ambayo ni tatizo la utafiti, malengo ya utafitiAthari ya Athari ya lugha ya Kiha katika ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili katika Shule za Msingi na Sekondari Wilayani Kasulu.

Malengo kuu na malengo mahususi maswali ya utafiti, mipaka ya utafiti, mipango ya utafiti, umuhimu wa utafiti, mawanda ya utafiti pamoja na mipango ya utafiti haya yataelezwa hapa

1.1.1 Lugha ya Kiha

Kiha ni lugha au kibantu ambacho kinapatikana Tanzania, ni miongoni mwa lugha ambazo zinaunda lugha ya wazungumzaji wa lugha hiyo wanaitwa waha na wazungumzaji wa lugha ya Kiha wapo wengi sana. Kiha ni lugha ya kibantu ambayo inapatikana magharibi mwa Tanzania na watu wanaozungumza Kiha wapo sehemu au mkoa wa Kigoma ambao upo magharibi mwa Tanzania. Kukua kwa lugha ya Kiha kumetokana na kuwa karibu na mpaka wa Tanzania na Burundi pia kutokana na uwepo wa njia nyingi za usafirishaji kwa njia ya maji, barabra na reli. Mkoa huu umepakana na nchi ya Burundi, mkoa wa Geita, Shinyanga Tabora, Kagera na Ziwa Tanganyika mpakani mwa nchi ya Jamuhuri ya Kidemokrasia ya Kongo.

1.1.2 Lugha ya Kiswahili

Swahili ni lugha ambayo ilianzia huko pwani, na Lugha hii ilikuwa ni mchanganyiko wa kibantu au vibantu vilivyokuwa vikizungumzwa huko. Kiswahili ni lugha ambayo ilianza kuzungumzwa ma watu wachache sana huko pwani ya Afrika Mashariki na ilisambazwa mpaka kufikia kuenea Tanzania nzima kama wimbi kubwa na waswahili wa Afrika Mashariki wakasambaza kiswahili sehemu tofauti tofauti kupitia biashara mbalimbali.

Lugha ya Kiswahili ni niongoni mwa lugha kubwa kwa ukubwa wake inafaa kabisa kuwa lugha ya diplomasia. Matumizi ya Kiswahili kidiplomasia yanafanya lugha ya Kiswahili kuenea kwa kasi kubwa sana kupitia wazungumzaji wengi kuliko ilivyo leo. Lugha hii huzungumzwa si tu Afrika mashariki na kati na kusini bali ulimwenguni kote na kufundishwa katika sehemu mbalimbali. Ni kweli kiswahili sasa kina nafasi ya kuwa lugha zinazotambuliwa Afrika na duniani kwa ujumla. (Ghanen 2005).

1.1.3 Muingiliano baina ya Lugha Mbili Tofauti

Lugha zaidi ya moja hutokea baada ya lugha mbili kuathiriana na kusababisha lugha hizo mbili kuchukua baadhi ya msamiati muundo mpaka maana kutoka katika lugha nyingine na kuweka katika lugha yake na lugha hizo hutokana na wanajamii wa lugha mbili tofauti kuishi katika jamii au sehemu moja. Na hapo ndipo lugha moja huanza kuchukua baadhi ya msamiati, sauti, maana na hata muundo kutokana na uchache wa msamiati wa lugha yake. Hivyo, hupelekea lugha ya Kiha kuingiliana na lugha ya Kiswahili.

Masebo na wengine (2008) wanaeleza kwamba Kiswahili kimeingiliana na lugha nyingi za kibantu kwa kuwa Kiswahili ni lugha ya pili katika jamii nyingi za kibantu.

Vile vile lugha za kibantu zimeathiri lugha ya Kiswahili hivyo Kiswahili na kibantu vimeathiriana kila lugha imaeathiri lugha nyingine kwa asilimia fulani.

1.2 Usuli wa Tatizo

Lugha ya Kiswahili ni lugha ambayo inatumiwa na watu wengi hasa katika nchi yetu ya Tanzania asilimia kubwa ya watu na makabila tofauti tofauti wanaopatikana katika sehemu mbali mbali hutumia lugha ya kiswahili katika kuwasiliana kwa kuwa ndio lugha ya taifa inayutumiwa na watu wengi hutumia katika mawasiliano. Ghanen (2005) ameeleza kuwa lugha ya Kiswahili ni moja kati ya lugha kubwa balani afrika na kutokana na matumizi yake makubwa huenea kwa kasi zaidi na kupata wazungumzaji zaidi.

Kutokana na wazungumzaji wa lugha ya kiha kama lugha mama yao kuanza kujifunza Kiswahili kama lugha yao ya pili imeleta mchanganyiko sana wa kifinolojia, kimofolojia, kisentakisia na hata kimaana kama lugha ya Kiswahili hiyo wazungumzaji wa lugha ya kiha huathiriwa sana na lugha yao na athari hizo huonekana pale wanapozungumza lugha ya Kiswahili.

Muingiliano wa lugha mbili tofauti huweza kuleta athari nyingi sana hasa lugha ya kwanza ndio huathiri lugha ya pili katika vipengele tofauti tofauti vya lugha. Katika utafiti huu. Mtafiti aliweza kuchunguza athari ya lugha ya kiha katika ufunzaji wa lugha ya Kiswahili katika shule za msingi na sekondari wilayani kasulu.

Watafiti mbalimbali walitafiti walitafiti athali za lugha mbalimbali katika lugha ya Kiswahili watafiti hao ni kama vile Asimwe Abel (2019) katika utafiti wake wa kuchunguza athiri ya kifonolojia za lugha ya kiha katika lugha ya Kiswahili hapa

aliangalia athari za lugha ya kiha iliyo athiri lugha ya Kiswahili kifonolojia pia Nyanda Joseph yeye alipofanya utafiti juu ya athari ya lugha ya kinyamwezi katika kufunza lugha ya Kiswahili huko Urambo. Mtafiti Joseph Ismaili Masasa katika utafiti wake yeye alichunguza athari ya lugha ya matamshi ya lugha ya kijita latika kufunza lugha ya Kiswahili na watafiti wengine pia walitafiti kuhusu athari za lugha ya kwanza katika lugha ya pili huyo kaitika tafiti hizo waliona kuonyesha athari hizo isipokuwa sijaiona tafiti aliyo tafiti athari ya lugha ya kiha katika kuathiri lugha ya Kiswahili kifonolojia, kimofolojia, kisintakisia, na pia kisematinki

1.3 Tatizo la Utafiti

Taratibu za lugha hutawaliwa na vipengele mbalimbali vya kisarufi. Watu hukosea sana kanuni za lugha ya Kiswahili kutokana na kuathiriwa na lugha nyingine. Watafiti waliotafiti kuhusu athari ya Lugha mama wameeleza athari za lugha moja katika kujifunza lugha ya pili kutokana na idadi wa watu wengi walioathiriwa na lugha ya Kiha wilayani Kasulu kuchanganya lugha Kiha katika lugha ya Kiswahili kimuundo, kimtindo, kimsamiati na hata kimaana ilipelekea Kiswahili kuathirika sana na kiha. Hivyo ilikuwa muhimu utafiti kufanyika ili kuweza kubaini tatizo hilo linalo athiri lugha ya Kiswahili na hili tatizo lakuwa na idadi ya watu wengi waliathiriwa na lugha ya kiha kushindwa kuzungumza Kiswahili fasaha ndilo lililopelekea mtafiti kufanya utafiti juu ya tatizo hilo. Lakini mpaka kufikia sasa hakuna uthibitisho kuhusu athari ya lugha ya Kiha katika ujifunzaji wa Lugha ya Kiswahili katika shule za Msingi na Sekondari Wilayani Kasulu miongoni mwa. Kwa Wanafunzi, Walimu, na Wanajamii Wengi wanaojifunza Kiswahili kama lugha yao ya pili kuna athari zinazotokea katika sauti, matamshi, muundo na maana. Kutokana na hayo yote upo

umuhimu wa kutafiti athari hizo na kubaini chanzo na jinsi kuondoa athari hizo na pia kubaini jinsi ya kuzuia athari hizo katika ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili.

1.4 Malengo ya Utafiti

Utafiti huu una malengo ya aina mbili ambayo ni lengo kuu na malengo mahususi.

1.4.1 Lengo Kuu

Kuchunguza athari za sarufi ya lugha ya Kiha katika ujifunzaji wa Lugha ya Kiswahili katika shule za Msingi na Sekondari.

1.4.2 Malengo Mahususi

i. Kubainisha athari za fonolojia, mofolojia, sintaksikia na semantiki katika ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili.

ii. Kubainisha sababu mbalimbali za lugha ya Kiha kuathiri ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili.

iii. Kutafuta njia za kutatua athari zilizopelekea lugha ya Kiha kuathiri lugha ya Kiswahili.(Lengo hili si sawa na ulivyoandika kwenye jedwali)

1.5 Maswali ya Utafiti

i. Lugha ya kiha ina athari gani za kifonolojia, mofolojia, kisintakisia na kisemantiki katika ufunzaji wa lugha ya Kiswahili
ii. Ni sababu zipi zinafanya lugha ya Kiha kuathiri lugha ya Kiswahili?
iii. Njia gani zitumike kuondoa athari za lugha ya Kiha ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili?

1.6 Umuhimu wa Utafiti

Utafiti huu una mchango mkubwa kitaaluma, kijamii, na kitamaduni kwa watu wote.

Kwa upande wa jamii, kupitia utafiti huu jamii itakuwa inafahamu athari mbalimbali za lugha ya Kiha katika lugha ya Kiswahili na itapelekea uhamasishaji wa uzungumzaji wa lugha ya Kiswahili sanifu, hivyo, idara ya Elimu itapelekea kuchapa na kuandaa vitabu vya uhamasishaji wa uzungumzaji wa Kiswahili sanifu kwa wanajamii mbalimbali ili Kiswahili kizidi kukua na kutumika kwa ufasaha.

Kitaaluma Utafiti huu utapunguza pengo au kuondoa kabisa pengo la utafiti juu ya athari ya Kiha katika lugha ya Kiswahili na utasaidia watu mbalimbali kutambua athari ya Kiha katika lugha ya Kiswahili na utawasaidia watu mbalimali kutambua athari na sababu na njia pia za kuondoa athari ya kibantu (Kiha) katika lugha ya Kiswahili na Watu hao ni wanafunzi, walimu, na wasomi mbalimbali.

Pia utafiti huu utawasaidia kuwasaidia watalaamu mbalimbali wa lugha ya Kiswahili kuweza kuelewa vizuri athari za lugha ya Kiha katika ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili na kuchukua athari chanya na kuziingiza katika lugha ili kuendeleza Kiswahili na pia kuangalia athari hasi na kuzifanyia kazi ili kutoa athari hizo katika ujifunzaji wa Kiswahili. Utafiti huu umekuwa na matokeo ambayo yatakuwa na manufaa ili kuweza kubaini makosa katika ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili kwa wanafunzi ambao wanaongea na wameaathiriwa na lugha ya Kiha ili kuondoa sababu zinazosababisha wanafunzi hao kuathiri Kiswahili katika ujifunzaji.

Utafiti huu utasaidia watafiti wengine watakao tafiti lugha nyingine

1.7 Mawanda na Mipaka ya Utafiti

Mtafiti anafahamu kuwa Kiswahili tayari kimeathiriwa kifonolojia, komofolojia na kisintakisia na lugha ya Kiha lakini kwa ufahamu wangu najua kuwa lugha hii ya Kiha

haitakuwa imefanyiwa utafiti juu ya kuathiri lugha ya Kiswahili. Mtafiti alitumia lugha mbili tu katika kufanya utafiti na kuona jinsi zinavyoathiriana katika Nyanja zote kisarufi, Kiswahili na kiha ndicho kilichotumika katika utafiti huu na sio vinginevyo.

1.8 Mpangilio wa Tasnifu / Muundo

Tasnifu hii ina sura tano. Sura kwanza ni utanguliz iusuli wa tatizo, malengo ya utafiti, maswali ya utafiti, umuhimu wa utafiti, mawanda na mipaka ya utafiti. Sura ya pili ni mapitio ya kazi mbalimbali yanayohusiana na mada hii ya utafiti, pengo la utafiti na nadharia ya utafiti, kihunzi cha nadharia, mfumo wa dhana na hitimisho. Sura ya tatu ni mbinu za utafiti, huku Sura ya nne ni uwasilishaji na uchambuzi wa data. Sura ya tano imetoa muhtasari wa utafiti hitimisho la utafiti na mapendekezo ya tafiti zijazo

SURA YA PILI

MAPITIO YA KAZI TANGULIZI

2.1 Utangulizi

Sura hii inaangalia mapitio ya kazi tangulizi kuhusiana na mada ya utafiti huu.

Mapitio hayo ni marejeo ya vitabu mbalimbali, machapisho mbalimbali na hata tafiti mbalimbali zinazohusiana na mada hii. Sura hii inaonyesha mitazamo mbalimbali ya watalaamu ulimwenguni waliofanya kazi zao kuhusiana na mada hii au inayokaribiana na mada hii ya utafiti. Kutokana na tafiti nyingi zilizofanywa hapo mwanzo kupitia watalaamu mbalimbali hapa ndipo litakapopatikana pengo la utafiti.

2.2 Mapitio ya Kazi Tangulizi

Mapitio ya kazi tangulizi ni mchakato wa kusoma kazi zilizopita za watalamu mbalimbali kuhusu mada hii ya utafiti. Mekacha (2011) katika utafiti wake uliohusu lugha moja kuathiriwa kutokana na muktadha wa matumizi yake alisema kuwa lugha kiswahili hutumiwa katika shughuli mbalimbali, kazini, ofisini, shuleni, biashara na sehemu zenye makutano ya watu wenye lugha mbili tofauti na kusema asilimia kubwa ya wanajamii wanapokuwa nyumbani hutumia lugha asili au lugha zao za kwanza na asilimia kubwa ya watanzania lugha ya kwanza ni kibantu cha eneo husika ijapokuwa wapo watu ambao lugha yao ya kwanza ni Kiswahili.

Hivyo, utafiti huu unamchango mkubwa ambao amesaidia kuonesha kuwa asilimia kubwa ya wanajamii hutumia lugha asili wawapo nyumbani na kuwa watanzania wengi lugha yao ya kwanza ni kibantu ambayo inapelekea kuathiri lugha yao ya pili ambayo ni Kiswahili, kwa asilimia kubwa wabantu wengi hujifunza Kiswahili kama lugha yao ya pili, isipokuwa haukuonesha moja kwa moja athari ya ya kiha katika

kujifunza Kiswahili. Selinker (1969) yeye aliona mifanyiko mitano ya kisaikolojia ni muhimu sana katika kuchunguza au kuangalia matatizo katika utumiaji wa lugha.

Mifanyiko hiyo ni kama, ujumlishaji mno kutokana na mfumo wa L1 inayotumiwa kiholela, uhamishaji wa kanuni za lugha ya kwanza hivyo kukiuka kanuni za lugha ya pili, mikakati ya mawasiliano kati ya lugha ya pili, njia za kujifunza zisizo halisi na uhamishaji wa ujifunzaji ambapo makosa hutokana na kutokuwa na umilisi kwa wanaofundisha. Makosa hayo yanaibua kiwango kingine katika matumizi ya lugha. Hivyo utafiti wa Selinker (1969) unashughulikia lugha kwa ujumla ututafiti wa sasa ulishughulikiwa lugha ya Kiha kwa kuangalia athari zake katika kujifunza Kiswahili.

Corder (1967) utafiti wake kuhusu lugha kadirifu na uchanganuzi wa makosa, katika utafiti huu Corder anasema, uchunguzi wa makosa una umuhimu kwa kuwa humuwezesha mtafiti kujua ambavyo watu hujifunza lugha fulani na mikakati wanayotumia katika mchakato wa kutambua lugha mara nyingi. Wanafunzi wanaojifunza lugha ya pili mara nyingi hukiuka sheria ya lugha ya pili, anaendelea kwa kusema kuwa matatizo yanapojitokeza anapojifunza lugha ya pili ni jambo la kawaida kutokea. Mwanafunzi hufanya makosa mbalimbali kwa lugha ya pili pale ambapo hajazoea matumizi ya sheria ya lugha ya pili.

Corder (1967) anasema makosa ni matatizo yanayotokea na utendaji na hivyo ni kikwazo chochote na yanaweza kutokea katika hali zozote. Corder (1967) anaeleza athari ya lugha ya kwanza kwenda katika lugha ya pili ambapo kulingana na utafiti wake bado hakuonyesha athari ya lugha ya Kiha katika ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili na hilo ndilo laweza kuwa pengo la utafiti wangu. Curtain (1990) katika utafiti wake kuhusu wanafunzi wanaojifunza lugha ya pili, anasema ni vyema kueleza

muundo na misingi mbalimbali ya lugha hiyo na pia matamshi bora. Uhusiamo kati ya lugha mbili ni muhimu sana kwa sababu huwa na muathiliano wa lugha hizo (Cook 1969) Pia anaendelea kusema kuwa lugha ya kwanza mara nyingi huathiri lugha ya pili, Kazi hii ina umuhimu sana katika kazi yangu kwa sababu inaeleza mwingiliano baina ya lugha mbili tofauti na hunesha jinsi lugha ya pili inavyoathiriwa na lugha ya kwanza. Hivyo, utafiti huu pia umenisaidia katika utafiti wangu pia kuangalia athari ya lugha ya Kiha katika ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili ijapokuwa wao hawakuangalia lugha ya Kiha hivyo hilo ni pengo kwa kuwa haikushughulikia lugha ya Kiha.

Nyangwine (2008) anaeleza kuwa lugha ya Kiswahili imeingiliana sana na lugha za kibantu na kwa kuwa lugha ya Kiswahili ina maneno mengi ya kibantu hivyo athari ya lugha ya kwanza inaonekana sana katika kuathiriana. Masebo na Nyangwine (2008) wao wanaeleza kuwa lugha ya Kiswahili imeingiliwa sana na lugha zingine za kibantu kwa sababu lugha ya Kiswahili ni lugha ya pili katika lugha nyingi za kibantu.

Athari ya pili lugha huonekana kwa kiasi kikubwa katika utamkaji. Pia lugha za kibantu zimeathiri sana lugha ya Kiswahili katika maana, matamshi, sauti, watu wengi sana hutumia lafudhi ya kikabila katika Kiswahili.

Kisakwah (2014) katika utafiti wake uliohusu uchunguzi wa kimakosa na muundo wa sentensi, ulinganisho wa sentensi za Kiswahili sanifu na kisuba, katika utafiti wake aliona makosa yanayofanywa na wanafunzi wengi katika uandishi wa insha na makosa hayo aliyachunguza katika vipashio vyote vya kiisimu mengi yalisababishwa na kuathiriwa na lugha ya kwanza kwa wanafunzi hao. Pia mtafiti huyo alibaini kuwa makosa yanayofanyika katika lugha ya pili yametokana na lugha ya kwanza lakini pia

ijapokuwa huu ulieleza athari hizo za lugha ya kwanza katika lugha ya pili ni dhahili kuwa haikuona athari ya lugha ya Kiha.

Masasa (2017) alitafiti athari ya matamshi ya lugha ya kijita katika kujifunza lugha ya Kiswahili, Katika utafiti wake alionesha athari mbalimbali za kimatamshi. Hivyo, kupitia utafiti huu amenisaidia mchango mkubwa sana katika utafiti wangu japokuwa yeye aliona athari katika lugha ya kijita na mimi naangalia athari ya lugha ya Kiha katika ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili, katika viwango vya hilo ndilo pengo la utafiti.

Richard na wenzake (1971) wanaeleza kuwa makosa ya kiisimu mengi hutokana na uhamisho kutokana na sababu mbalimbali, vipengele mbalimbali vya kiisimu vinaweza kuhamishwa kutoka lugha moja kwenda lugha nyingine, kutoka lugha ya kwanza kwenda lugha ya pili na hivyo huanza kuathiri mfumo wa lugha ya pili. kupitia utafiti huo mtafiti hakuweza kuonesha athari za lugha ya Kiha katika lugha ya Kiswahili ingawa kaonesha athari ya lugha ya kwanza katika kuathiri lugha ya pili na hilo ndilo pengo la utafiri huu.

Otiende (2013) katika utafiti wake ameangalia athari ya lugha ya kwanza katika kujifunza lugha ya pili, yeye aliangalia sana michakato ya kofonolojia katika kisuba ba Kiswahili sanifu, kupitia utafiti wake ameonesha tofauti kubwa ya kifonolojia kati ya kisuba na Kiswahili, ambazo tofauti hizo huathiri lugha ya Kiswahili na hivyo mtafiti hajasema chochote kuhusu lugha ya koha na hilo ndio sehemu ya utafiti huu.

Kutokana na mapitio ya kazi tangulizi hapo juu ni kweli kuwa mwingiliano wa Lugha mbili au zaidi husababisha lugha moja kuathiri lugha nyingine kimuundo, kimaana, kisauti na hata kimatamshi. Lugha moja inaweza kuchukua baadhi ya misamiati

miundo matamshi hata sauti kutoka katika lugha nyingine, na hali hii hutokea mara nyingi mtu au kundi la watu linapojifunza lugha Fulani kama lugha ya pili kwao. Kutokana na kuwa lugha hio wanayojifunza kuwa ngeni au kuwa lugha ya pili huchukua baadhi ya maneno muundo maana na hata sauti ya lugha yao ya kwanza na kuweza kutumia katika lugha ya pili.

2.3 Maana ya Istilahi Zilizotumika Kwenye Utafiti

Kutambua tafsiri ya lugha kutokana na kwamba Lugha imefasiliwa na watalaamu mbalimbali kama ifuatavyo;

2.3.1 Lugha

Habwe na Kalanja (2004) wakinukuu TUKI (1990) wanasema kuwa lugha ni mfuno wa sauti za nasibu zinazotumiwa na watu wenye utamaduni unaofanana ili kuwasiliana. Masamba na wenzake (2009) wanadai kuwa lugha ni mfumo wa sauti za nasibu ambazo zimebuniwa na jamii moja kwa madhumuni ya mawasiliano kati yao.

Crystal (1992) anasema lugha ni mfumo wa sauti za nasibu, ishara na maandishi kwa ajili ya mawasiliano ya kujieleza katika jamii ya watu. Hivyo basi tunaweza kusema kuwa lugha ni mfumo wa sauti za nasibu zinazokubaliwa na jamii moja ili zitumike kama mawasiliano baina ya jamii hizo.

2.3.2 Lugha Asili

Masanja na wenzake (2009) wanasema lugha asili ni lugha inayotokana na wanajamii wa eneo fulani ambao wanamila, desturi na utamaduni wa aina moja. Lugha ya asili hueleza mambo ya asili na desturi kwa kujitosheleza. Lugha asili tunaweza kusema kuwa ni lugha ambayo ilikuwa kama sehemu ya utamaduni wa uma fulani ambayo

inauwa kama lugha mama. Hivyo lugha ya asili ni lugha ambayo hutumiwa na watu wanaokaa katika eneo moja na wenye utamaduni, desturi, mila na mtindo mmoja wa maisha.

2.3.3 Lugha Ya Pili

Masanjila na wenzake (2009) wanasema kiwa lugha ya pili ni lugha anayojifunza mtu baada ya lugha yake ya kwanza au lugha mama. Kimsingi lugha ya pili huwa ni lugha rasmi imumikayo katika utawala wa serikali. Masebo na Nyangwine (2008) lugha ya pili ni lugha ambayo binadamu hujifunza badala ya lugha ya kwanza. Kiswahili ni lugha ya pili kwa watanzania wengi.

Hivyo tunaweza kusema lugha ya pili ni lugha ambayo mtu hujifunza baada ya lugha ya kwanza. Na katika hili Kigoma, Kiswahili ni lugha ya pili kwa watu wengi waishio huko lugha yao ya awali ni Kiha.

2.3.4 Ujifunzaji Lugha

Masamba (2004) anadai kuwa ujifunzaji lugha ni utaratibu wa kufanya jitihada rasmi za kujua na kutumia lugha fulani. Mtu huwa na uwezo wa kujifunza na kufahamu akiwa tu na akili timamu. Upangaji wa sauti zote zinazohusiana na ujifunzaji wa lugha.

Ujifunzaji wa lugha ya pili hutokea katika mazingira mbalimbali. Wapo wanaojifunza lugha ya pili kwa urahisi sana kwasababu ya mazingira ya sehemu anayojifunza lugha hiyo.

2.4 Pengo la Utafiti

Wataalamu na watafiti mbalimbali kama vile, Joseph Ismail Masasa (2017), Miza Hasan Faki (2018), Nyanda Josephine (2015) walitafiti athari ya lugha ya kwanza au

awali katika kuathiri lugha ya pili katika kujifunza lugha ya Kiswahili. Pia watafiti wengine wameangalia athari za vibantu vingine katika ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili, hivyo mpaka kufika leo hii hakuna utafiti uliochunguza athari ya lugha ya Kiha katika ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili katika Shule za Msingi na Sekondari, na hilo ndilo pengo la utafiti huu. Pengo la utafiti huu ni kuweka wazi athari za Lugha ya Kiha katika ujifunzaji wa Lugha ya Kiswahili pamoja na kutafuta chanzo cha athari hizo na jinsi ya kuondoa athari hizo.

2.5 Kihunzi cha Nadharia

Wamitila (2011) anaeleza kuwa nadharia ni mawazo, dhana au maelezo yanayotolewa kueleza hali fulani, chanzo chake, utendaji kazi wake na mwingiliano wake wa ndani na nje. Masamba (2004) anasema kuwa nadharia ni kanuni na misingi ambayo hujengwa katika msingi wa mawazo ili kutumiwa kielelezo cha kueleza jambo fulani. Wafula na Kimani (2007) wanasema kuwa nadharia ni istilahi ya kiujumla inayomaanisha miongozo inayomuelezea msomaji au muhakiki wa kazi fulani ya lugha, fasihi na isimu kufahamu kazi hio na vipengele vyake. Hivyo, naweza sema nadharia ni mawazo kiujumla yanayoelezea msomaji wa jambo fulani.

2.6 Nadharia ya Mawasiliano

Nadharia ya ethnografia ni nadharia iliyoasisiwa na Dell Hyme Mwanaathropolojia kutoka Marekani, nadharia hii inafanya kazi ya kutambua mazingira halisi ya kitamaduni na kimuktadha ambapo mawasiliano hufanyika. Pia huchanganua matini za mawasiliano wanapozungumza. Utafiti huu umeongozwa na nadharia ya mawasiliano. Nadharia hii ina lengo la kukuza lugha na kuweka mikakati mizuri kwa wale wanaojifunza lugha ya pili katika kuwasiliana. Lengo la nadharia hii ni kukidhi

mahitaji ya kuwasiliana au matakwa ya wanaojifunza lugha ya pili. Pia dhana hii inataka kuimarisha mbinu za ujifunzaji. Kutokana na mada hii ya utafiti mtafiti ametumia nadharia ya mawasiliano ambayo iliasisiwa na Giles (1973). Nadharia hii ilipewa jina la nadharia ya ulinganisho wa lugha ama mawasiliano.

Utafiti wa nadharia hii ya Giles ulibaini kuwepo kwa mabadiliko ya kisarufi kama sauti, matamshi, muundo na hata maana kwa wazungumzaji walio wengi. Na alipenda chanzo cha tatizo hilo. Nadharia hii ilikuwa na lengo la kubadili mtindo wa kimatamshi katika mawasiliano kwenye jamii pamoja na kutambua athari zake.

Watu huweza kujaribu kuibua aina fulani ya mwigo wa matamshi na sauti fulani kutoka kwa watungumzaji wengine ilimradi wakidhi haja ya mawasiliano baina yao, na watu hao hufanya mwigo huo kwa kutarajia au kutokutarajia, na mwigo huo wa vipengele vya kisarufi vya lugha hutokea kwa watu wanaozungumza pamoja. Dhamira ya nadharia hii ni kuonesha sababu za kubadili mtindo na vipengele vingine vya lugha ndani ya mawasiliano katika jamii fulani pamoja na kuangalia athari zake ndani ya jamii hiyo.imetumia nadharia hii ya Giles (1973) katika utafiti wangu kwa kuwa nadharia hii inakidhi matarajio ya utafiti.

2.7 Mfumo wa Dhana

Miles na Huberman, (1994), wanasema kuwa mfumo wa dhana ni uhusiano kati ya dhana zinazotafitiwa kwa kuangalia vipengele muhimu kama vile sababu, dhana au kutofautiana kwa mawazo yanayodhaniwa kwa njia ya vielelezo au maandishi. Tofauti ya kujitegemea hupelekea kuwepo Kwa tofauti tegemezi. Katika tafiti hii vielelezo vya tofauti ya kujitegemea na tofauti tegemezi vimeainishwa ili kuonesha sababu moja inayopelekea nyingine.

2.7.1 Tofauti ya Kujitegemea

- Mwingiliano wa lugha ya kiha katika Kiswahili
- Kuathiriwa kwa Lugha mama
- Kutofahamu baadhi ya misamiati ya lugha ya Kiswahili

2.7.2 Tofauti Tegemezi

- Kuchanganya lugha katika muktadha wa:
  - Kimuundo
  - Kimtindo
  - Kimsamiati



Kielelezo Na. 2.1: Tofauti ya Kujitegemea

Chanzo: Mtafiti, 2022

2.8 Hitimisho

Sura hii imepitia mapitio ya kazi tangulizi mbalimbali ambayo yameeleza athari ya Lugha ya kwanza inavyoathiri lugha ya pili. Japo kuwa siyo wataalam wote wameeleza jinsi lugha ya kwanza ilivyoathiri lugha ya pili, wapo pia wataalamu na watafiti waliotafiti athari ya lugha mbalimbali ikiwa kama lugha ya kwanza

ilivyoathiri lugha ya pili kwa watu wa lugha hio. Athari hizo zilizochunguzwa ni pamoja na athari za kimofolojia, kifonolojia, kisntaksia na kisantaksia katika lugha tofautitofauti.

Hivyo utafiti huu utatafuta athari ya Lugha ya Kiha katika ujifunzaji wa Lugha ya Kiswahili kwa kupitia nadharia ya mawasiliano ambapo nadharia hii inaonyesha sababu za kubadili mtindo na vipengele vingine vya Lugha ndani ya mawasiliano katika jamii fulani pamoja na kuangalia athari zake ndani ya jamii hiyo. Hii imepelekea nadharia hii kuichagua ili kusaidia mtafiti kufanya Utafiti wake.

SURA YA TATU

MBINU ZA UTAFITI

3.1 Utangulizi

Kothari (2008) anasema kuwa utafiti wowote wa kitaaluma lazima ufanywe kwa kuongozwa na mbinu mbalimbali za utafiti ili kutoa matokeo yasiyo na shaka ndani yake. Sura hii imeeleza mbinu mbalimbali ambazo zimetumika katika utafiti huu

3.2 Mkabala wa Utafiti

Mkabala ni utaratibu, mtazamo au kanuni katika kuhakiki kazi za fasihi (Ghanen 2005). Mitazamo ya wahakiki wa kazi za fasihi hutofautiana baina ya mhakiki mmoja na mhakiki mwingine. Takwimu huchanganuliwa kwa kutumia mikabala mikuu mitatu, ambayo ni kiitikadi, mkabala wa kimaelezo (au usio wa kiitikadi) na mchanganyiko. Mkabala wa kiitikadi huweza kuchanganuliwa kwa kutumia takwimu. Enon (1998) anaeleza kwamba mkabala usio na kiitikadi ni mbinu ya kuchunguza takwimu ambayo mtafiti hueleza na kufafanua data zake kwa kutumia maelezo.

3.2.1 Mkabala wa Kimaelezo

Huu ni mkabala ambao mtafiti hutumia maelezo katika kutoa majibu yake ya utafiti.

3.2.2 Mkabala wa Kitakwimu

Huu ni mkabala ambapo mtafiti huweza kutoa majibu ya maswali ya utafiti kwa kutumia namba au takwimu.

3.2.3 Mkabala wa Mchanganyiko

Mkabala Mchanganyiko ni mkabala ambao unatumia mikabala miwili yaani mkabala wa kitakwimu na mkabala wa kimaelezo katika ukusanyaji wa data. Mchanganyiko ni

umoja wa vitu viwili au zaidi au vitu ambavyo vinaweza kupatikana katika hali yoyote ya jambo, kulingana na hali ya vitu. Mchanganyiko unaweza kuwa wa muziki, kijamii, kimwili, kikemikali au vitu vingine.

Katika utafiti huo mtafiti alitumia mkabala mchanganyiko katika kuchambua data zake. Mtafiti alitumia mkabala huu kwa sababu kuna baadhi ya takwimu zitahitaji maelezo au zitahitaji kuandikwa kwa maelezo.

3.3 Eneo la Utafiti

Ngure (2011) anasema kwamba inabidi kuamua ni wapi utakusanya takwimu ni muhimu sana kuchagua sehemu ya kukusanyia takwimu hizo. Uchunguzi huu ulijikita katika mkoa wa Kigoma katika wilaya ya Kasulu kata ya Lusesa. Mtafiti alichagua kata hiyo kwa kuwa wanajamii katika eneo hilo ndio wanaoathirika sana na kibantu na katika hili asilimia kubwa ya wanajamii wameshindwa kuongea kiwsahili fasaha, mtafiti alichagua eneo hilo kwa kuwa kabla ya tafiti aliona yeye mwenyewe kuwa wanajamii wameathiriwa sana na lugha mama

3.4 Uteuzi wa Walengwa

Kothari (2004) anasema kwamba uteuzi wa walengwa ni mbinu au utaratibu ambao mtafiti alitumia katika kuchagua orodha ya watu kwa ajili ya sampuli kutokana na utafiti huu walengwa watakuwa ni watafutiwa yaani wanajamii wa mji wa kigoma na walengwa hasa ni wanajamii wa mji wa Kigoma yaani waha na wataalamu wa lugha ya Kiswahili. Willman (2011) anaeleza kua walengwa ni jumla ya vitu vyote vinavyohusika katika utafiti, yaani watu, taasisi, vitu au matukio. Kwa sababu hiyo walengwa ni wote au vyote ambavyo mtafiti au sampuli amechagua ili kuweza kuleta data sahihi. (Copper na Vans 1989) wanasema kuwa kundi lengwa ni wanachama

wote, mtu mmoja, Kukindi au elementi ambazo anamsaidia mtafiti msaidizi kuhusisha takwimu katika utafiti wake kwa mujibu wa Ingule (1988) anasema kuwa uchaguzi usio wa kukusudia ni ule ambao mtafutiwa huteuliwa kutokanana vigezo alivyonavyo au taarifa aliyonayo kuhusu utafiti unaofanyika. Hivyo, utaratibu wa kuwapata watafitiwa huweza kuwa ni uteuzi wa walengwa na uteuzi huo upo wa njia tofauti tofauti; kuna mbinu ya kukusudia na mbinu ya kutokuwasaidia. Hivyo mtafiti alitumia njia ya kukusudia kuteua walengwa.

3.4.1 Sampuli na Usampulishaji

Mtatifi aliteua sampuli ya watafitiwa kulingana na wa kutoa ambazo zinahitaji kupata mtafiti na watafutiwa ambao wana uwezo wa kutoa habari juu ya utafiti husika kwa usahihi. Sigh (2007) anaeleza kuwa usampulishaji ni mchakato wa kuchagua kundi dogo kutoka katika kundi kubwa la watafitiwa ili kufanya makisio ya walengwa. Babbie (1992) yeye anadai kuwa sampuli sehemu dhidi ya watu ambao mtafiti anavutiwa nayo katika kupata taarifa ambayo ni hitimisho la utafiti wake.

Utafiti huu ulihusisha walimu 10 kutoka shule ya sekondari na msingi wanaofundisha Kiswahili, wanafunzi 20 kutoka shule ya sekondari ambao ni wamilisi wa lugha ya Kiha na wanajifunza Kiswahili, wanafunzi wa darasa la 1 kutoka shule ya msingi ambao hawajui Kiswahili yaani wanajifunza Kiswahili na wamilisi wa Kiha pamoja na wanajamii wanaotumia kilugha 15 au wamlisi wa lugha ya Kiha lakini pia wanaongea Kiswahili. Walengwa wote hao walichaguliwa kwa makusudi nilitumia usampulishaji huo nikiamini kuwa utaleta matokeo mazuri ya utafiti.

Jedwali Na. 3.1: Mchanganuo wa Watafutwa

Namba	1	2	3	Jumla
Kundi la watafutwa	Walimu wanaofundisha shule ya msingi na sekondari	Wanafunzi wa sekondari na msingi	Wanajamii wanaojua Kiswahili	
Idadi	10	20	15	45

3.5 Vyanzo vya Data

Kuna aina tofauti tofauti za data. Muligo (2012) anasema kuwa kuna aina kuu mbili za data ambazo ni data za msingi au awali na data za upili au sekondari.

3.5.1 Data za Msingi au Awali

Hizi ni data ambazo zinapatikana kupitia kwa mtafiti mwenyewe na ni data ambazo zinakusanywa kwa mara ya kwanza na mtafiti na zinazotoka kwa watafitiwa wenyewe.

3.5.2 Data za Upili

Data za upili hizi zinapatikana kupitia machapisho mbalimbali kama vile vitabu na makala na majarida mbalimbali yanayohusu au kukaribiana na mada husika ya utafiti. Ili kupata data za upili za utafiti ilimbidi mtafiti asome makala na vitabu mbalimbali.

3.6 Ukusanyaji wa Data

Kombo na Tramp (2006) wanasema kuwa ukusanyaji wa data unahusu kukusanya taarifa, maarifa mahususi zilizokusudiwa kutoa au kupinga uhalisia wa jambo fulani. kupitia utafiti huu taarifa zilizokusanywa zilikusanywa kwa kuwa na taarifa za uwandani yaani kupitia watafitiwa na taarifa za maktaba yaani taarifa mbalimbali zilizopatikana kupitia kusoma makala na vitabu mbalimbali katika maktaba.

3.6.1 Vifaa vya Kukusanyia Data

Mtafiti alindaa vifaa mbalimbali vya kukusanyia data kulingana na utafiti huu. Mtafiti alitumia noti buku na peni, Vifaa hivi vilimsaidia mtafiti kuandika na kunukuu taarifa muhimu kupitia mahojiano, mahali walipokuwa wanahojiana na yapi yalizungumzwa katika mahojiano hayo. Hizo ni data za msingi ambazo zilinukuliwa na mtafiti na kuandikwa katika noti buku na karatasi. Pia mtafiti alitumia kompyuta, kutafuta matini mbalimbali na mapitio ya kazi mbalimbali kwa kuanzia mwanzo wa utafiti hadi mwisho wa utafiti, Pia kompyuta ilitumika kuhifadhi matini yaliyotumika wakati wa kukusanya data. Kinasa sauti pia kilitumika kuchukua sauti mbalimbali katika kukusanya data.

3.6.2 Mbinu za Ukusanyaji data

Katika sehemu hii mtafiti anapaswa kutumia au kuchagua mbinu nzuri ya kukusanyia data. Pia anapaswa kutumia njia sahihi ambayo anaona kuwa njia hio inaweza kuleta majibu mazuri katika maswali yake ya utafiti, Hivyo, mtafiti huweza kuchagua mbinu ya kusadanya data kutokana na mada ya utafiti iliyo pamoja na maswali yake ya utafiti jinsi yalivyo. Kothari (1990) anaeleza kuwa ukusanyaji wa data ni zoezi la awali katika utafiti ambao humuwezesha mtafiti kupata taarifa ambazo zitamsaidia kumfikisha kwenye malengo aliyojipangia.

Msoghaa (2010) anaeleza kuwa ni lazima kuhakikisha kuwa mbinu za utafiti zinatoa aina ya taarifa zinazohitajika kujibu maswali utafiti husika. Pia, Kothari (1990) anaendelea kusema kuwa lazima itangulie hatua ya kukusanya data ndipo hatua zingine kama uwasilishaji na uchanganuzi wa data zifuate Kupitia hayo, mtafiti alitumia mbinu mbalimbali za kukusanya data zilizomsaidia kufikia malengo yake.

Mtafiti alitumia mbinu ya hojaji, mahojiano na majadiliano ili kukidhi haja ya utafiti wake.

3.6.2.1 Mahojiano au Usaili

Kothari (1990) anasema kuwa mbinu hii inaruhusu kutumia maswali mbalimbali kwa watafitiwa. Mbinu hii ya kuuliza maswali mbalimbali yanayohusu utafiti husika yanaweza kuwa kwa njia ya ana kwa ana au mawasiliano kwa njia ya simu. Mawasiliano hayo yanaweza kuwa baina ya mtu na mtu au kundi la watu fulani kwa nia ya kupata data za utatiti. Mtafiti alitumia mwongozo wa maswali mbalimbali ili kumuongoza katika mahojiano mbalimbali baina ya mtafitiwa na mtafiti au baina ya mtu na mtu. Watafitiwa waliulizwa maswali mbalimbali na wakijibu mtafiti alinukuu katika noti buku. na karatasi. Mbinu hii ina faida kama vile kupata ufafanuzi wa data kupitia ana kwa ana na inampa utafiti kuweza kuuliza maswali zaidi kama itahitajika. Mtafiti alitumia njia hii ya usaili au mahojiano kwa walimu, wanajamii na wanafunzi. Aliuliza maswali kadri awezavyo ili kutimiza malengo yake ya utafiti. Kothari (2004) anaeleza kuwa njia hii hutumika kukusanya data na kuwasilishwa kwa njia ya mdomo ana kwa ana baina ya mtafitiwa na matafiti.

Mbinu hii ilimwezesha mtafiti kupata data za awali ambazo zilitokana na watafiti wa kujibu maswali walio ulizwa na mtafiti liategemea. Mbinu hii humsaidia mtafiti kuelezea vizuri maswali aliyotarajia kuuliza kwa watafitiwa ili watafitiwa waelewe vizuri na kujibu maswali vizuri. Njia hii ina faida kwa sababu inaweza kutoa majibu ya papo kwa papo. Pia, mtafiti anaweza kutambua kuwa majibu yanayotolewa yana ukweli au hayana ukweli kulingana na watafitiwa watakavyojibu maswali.

3.6.2.2 Hojaji

Baraza la Kiswahili la Zanzibar (2010) linasema kuwa hojaji ni karatasi ya maswali ya utafiti kuhusu jambo maalumu. Mbinu hii huweza kuandaa maswali yanayohusu utafiti na kuwapa watafitiwa. Maswali hayo huwa yameandikwa katika karatasi. Maswali hayo yanaweza kuwa ya kujibu kifupi ama kujieleza hata kuchagua. Buliba (90) anasema hojaji ni seti ya maswali yanayoandaliwa au kauli zinazohusiana na suala linalotafitiwa ambalo mtafiti hutoa kwa wahojiwa kwa ajili ya kubaini habari, majibu, maoni, mitazamo na mikabala mahususi kuhusu mada ya utafiti na maswali hayo ya hojaji yanaweza kuwa maswali ya wazi au yasiyo ya wazi (funge). Mtafiti aliandaa maswali mbalimbali katika karatasi kulingana na idadi ya watafutiwa na maswali hayo yalikuwa ya wazi na mengine haya kuwa ya wazi. Watafitiwa waliotumiwa katika kujibu maswali haya ni wanafunzi na walimu walio chaguliwa kama sampuli.

3.6.2.3 Majadiliano

Majadiliano ni njia ya mawasiliano ya kuchangia mawazo kati ya watu wawili au zaidi. Njia hii huweza kusaidia mtafiti kupata taarifa za uhakika. Mtafiti ametumia njia ya majadiliano kati ya mtafiti, na wanajamii na mtafiti na wanafunzi Mtafiti alibaini kuwa athari ya lugha mama ndio chanzo kikuu cha lugha ya kiha kuathiri lugha ya kiwsahili ijapokuwa pia alipata ayhari nyingine zilizopelekea lugha ya kiha kuathiri lugha ya Kiswahili. Tatabi (2013) anasema kuwa majadiliano ni mazungumzo kati ya watu wawili au zaidi wanaobadilishana mawazo ambayo mtafitiwa kutoa haraka taarifa au habari nyingi nzuri za kufaa. Mtafiti alitumia mbinu ya majadiliano kupata data za uwandani.

3.7 Uhalali na Uthibiti wa Matokeo ya Utafiti

Uhalali – hiki ni kiwango cha namna ya kifaa kinaweza kupima kile kusudia kupima mugedi. 2003. Uhalali ni kiwango kinachopanua kutokana na uchanganuzi wa data na namna kinavyowakilisha mada inayotafitiwa. Katika tafiti hii mtafiti alitunia watafiti mbali mbali waliotafiti juu ya Kiswahili na lugha nyingine. Maswali yaliyo andikwa kwaajili ya kujibiana kama hojaji yalikaguliwa kwa msimamizi na kuona yanafaa katika kuleta taarifa zilizo kusudiwa na mtafiti pia vifaa vilivyotumika kukusanya data vilionekana kuwa sahihi.

3.7.1 Maadili ya Utafiti

Mtafiti alihakikisha amepata kibali kutoka chuoni kibali cha kufanya utafiti kaktika mkoa wa kigoma wilaya ya kasulu kibali huhicho kilipitia katika tawala za mikoa na serikali za mitaa (TAMISEMI) Baada ya hapo mtafiti alipewa kibali cha kupeleka mkoani kigoma na huko pia mtafiti alipewa kibali cha kupeleka wilayani na huko kulipatikana kibali cha kuwafikishia waalimu wakuu wa shule alizoteua mtafiti ili kufanya utafiti hapo wanafunzi walipewa taarifa na baadae mtafiti aliendа mashuleni kufanya utafiti na hapo walielezwa kuwa data watakazozitoa zitakuwa ni siri ya mtafiti na wanafunzi hazitasambazwa sehemu yoyote wala kusema nani alisema nini. Na watafiti waliambiwa data hizo zitatumika kwa siri ya utafiti tu na sio vinginevyo.

3.7.2 Uthabiti

Ni kiwango ambacho mtafiti hupima matokeo yake kama ni ya kweli au sio ya kweli katika utafiti huu mtafiti amethibitisha watafiti wakitoa maelezo ambayo ni ya uhakika kwakuwa hakuwalazimisha kutoa taarifa hizo bali walitoa matokeo ya athari ya lugha ya kiha katika ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili wakiwa na uhuru pasi na

kulazimishwa. Hata hivyo mtafiti aligundua kuwa matokeo yale ni thabiti kwakuwa katika dodoso zake majibu yaliyokuwa yakijibiwa na watafiti yalikuwa yakifanana au kukaribiana ingawa watafiti hao walipewa dododso huizo kwa muda na siku tofauti tofauti. Majibu yaliyotolewa na watafiti hao yalikuwa yanakalibiana na hapo mtafiti aligundua kuwa majibu hayo ni thabiti

3.8 Hitimisho

Sura hii imeeleza vipengele mbalimbali vya utafiti kwa undani kama vile sampuli na usampulishaji, mbinu za ukusanyaji wa data ambapo mtafiti ametumia mbinu ya mahojiano au usaili ambayo ilimsaidia mtafiti kuuliza maswali mengi zaidi kadri anavyoweza. Pia, ametumia mbinu ya hojaji mbinu hii imetumika kwa kuwa huumpa uhuru mtafitiwa wa kuandika kile anacho kifahamu pasipo woga. Mbinu nyingine aliyotumia mtafiti ni majadiliano. Mbinu hii ilimsaidia mtafiti kujadili mambo mengi zaidi kuhusu utafiti wake. Mbinu hizi zinafaa kwa kuwa zimeleta majibu yaliyotarajiwa na mtafiti tofauti na mbinu zingine zilizobaki kama vile ushuhudiaji unaweza kusababisha kukosa baadhi ya data zinazohitajika katika utafiti.

SURA YA NNE

UWASILISHAJI, UCHAMBUZI NA MJADALA WA DATA ZA UTAFITI

4.1 Utangulizi

Surah hii ilihusisha taarifa zilizokusanywa wakati utafiti huu ulipofanyika.Utafiti huu ulihusisha Kijiji cha Lusesa Mkoani Kigoma ambapo katika Kijiji hiki Utafiti huu ulihusisha Shule mbili za Msingi na shule mbili za sekondari pamoja na Wanakijiji. Utafiti huu ulitumia makundi matatu katika kukusanya taarifa hizi.Makundi hayo ni Walimu, Wanafunzi, pamoja na wanakijiji ambao jumla **45;** walikuwa walimu 5 wanaofundisha shule ya Msingi, na walimu 5 wanaofundisha Shule ya Sekondari, Wanafunzi wa Sekondari 10, kati yao wasichana 5, na wavulana 5. Wanafunzi wa Shule ya Msingi 10; wavulana 5 na wasichana 5 pamoja na Wanajamii 15 wanaofahamu Lugha ya Kiswahili vizuri.

4.2 Majibu ya Maswali ya Utafiti

4.2.1 Athari ya Lugha ya Kiha Katika Ujifunzaji wa Lugha ya Kiswahili

Lugha mama au Lugha ya kwanza mtu aliyojifunza huwa na athari katika ujifunzaji wa Lugha ya pili. Lugha ya pili yaweza kuwa ni lugha yoyote ile ila iwe ya pili kujifunza. Yaweza kuwa ni Kiswahili au Kiingereza mtu anayejifunza lugha ya pili huwa na vikwazo vingi ambavyo humfanya kushindwa kuwasiliana vizuri kwa kutumia lugha ya pili au huwa na vikwazo katika upande wa pili huonesha udhaifu wa mawasiliano hasa katika lugha ile anayojifunza. Athari za lugha ya Kiha katika ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili katika shule za msingi na sekondari ni kama zifuatazo;

4.2.2 Kuongezeka kwa Baadhi ya Viambishi Visivyohusika

Wanafunzi wanaongea lugha ya Kiswahili walioathiriwa na Lugha ya Kiha. Huongeza viambishi mbalimbali katika maneno ya Kiswahili sehemu isiyohusika ili kukidhi haja ya mawasiliano. Hivyo, inaweza kutokea katika matamshi au hata katika msamiati kuongeza baadhi ya viambishi visivyotakiwa. Kiini cha taarifa hii imetoka katika majibu waliyojibu watafitiwa ambao ni walimu, wanafunzi pamoja na wanajamii.

Kutokana na majibu yaliyotolewa na makundi ya watafitiwa, Waha wengi huongeza baadhi ya viambishi katika misamiati na maneno ya Kiswahili na viambishi hivyo vinavyoongezwa ni kama vile ng'o, ga, ge, po ambapo vitenzi hivi hutokea baada ya Utamkaji wa Kitenzi kumalizika ndipo viambishi hivyo huwekwa katika msamiati ya Kiswahili.

Kwa Mfano:-

1. Twende -Tugendapo
2. Nenda – Gendapo
3. Nenda – Gendapo
4. Pika – Teka –ga
5. Njoo – Ingo
6. Kula – Laya-ga
7. Kaa – Ichala-ga
8. Lala – Lala-ga

Hivyo wanafunzi wengi wa Kiha huweka viambishi kama hivyo katika msamiati wa Kiswahili. Tazama jedwali hapo chini.

Jedwali 4.1: Kuongezeka kwa Baadhi ya Viambishi Visivyohusika

Misamiati ya Kiswahili	Silabi zinavyoongezwa na wazungumzaji wa lugha ya Kiha.
Twende	Twenda-ge
Nenda	Nenda-ga
Beba	Beba-ga
Cheza	Cheza- ga
Nenda	Nenda-po
Kula	Kulaga –ga
Lala	Lala –po
Sikia	Sikia-ga
Pika	Pika-po
Lia	Lia –po
Soma	Soma –po
Tunakula	Tunakula-ga
Amelima	Amelima-po
Songa	Songa-ge
Nipe	Nipe-po
Andika	Andika-po
Piga	Piga-po

Kwa hiyo, wazungumzaji wa lugha ya Kiswahili fasaha wakisikia utamkaji wa lugha ya Kiswahili kama hivyo hufahamu kabisa kuwa wazungumzaji hao, sio wamilisi wa lugha ya Kiswahili kwa kuwa wameongeza viambishi ambavyo havitakiwi katika Msamiati wa lugha ya Kiswahili kutokana na kuathriwa na lugha mama yao. Pia, athari hizo huonekana pale anapotamka neno/Msamiati huo mtu aliyeathiriwa na lugha

ya Kiha hutamka misamiati kwa kukaza au kukandamiza sana maneno ni tofauti na mtu ambae hajaathiriwa na Lugha hio na mtu anaeweza kufahamu utofauti huo ni yule ambae anafahamu vizuri Kiswahili Sanifu: Kihore (2009) alieleza kuwa utaratibu wa mpangilio wa viambishi huwa katika mfuatano unaotupatia silabi zilizokubalika katika lugha kwa mfano:-

Anakula

a- Na- kul- a

a- Kiambishi awali nafsi ya tatu umoja

na - kiambishi cha njeo (wakati uliopo)

Kul – mzizi wa neno

a – kiambishi tamati.

Anacheka

a – kiambishi awali nafsi ya tatu umoja

na – kiambishi cha njeo wakati uliopo

chek – kiini cha neno

a – kiambishi tamati

Idarusi (2005) anaonesha athari zinazojitokeza katika lugha ya Kiswahili baada ya Wanafunzi kuathiriwa na lugha ya kwanza. Athari hizo ni pamoja na makosa ya muundo wa sentensi makosa ya matamshi sauti pamoja na msamiati.

4.2.3 Uelewa Mdogo wa Wanafunzi Wakati wa Ufundishwaji

Athari ya lugha ya Kiha katika ufunzaji wa lugha ya Kiswahili ni pamoja na wanafunzi kutokuelewana vizuri na mwalimu. Chacha (2011) anasema kuwa lengo la nadharia ya mawasiliano ni kukuza uwezo wa kuwasiliana, hivyo kutokana na data katika maswali ya baadhi ya makundi ya watafitiwa ambalo swali hiloliliuliza kuwa “Mkiwa

nyumbani huwa mnatumia lugha gani katika kuwasiliana?" na majibu yao asilimia kubwa hutumia lugha ya Kiha. Rocha 2011. anaeleza kwamba wabantu wengi wameathiriwa na lugha mama.Watafitiwa wengi katika makundi ya watafitiwa walipoulizwa ni ipi lugha mama yako kati ya Kiswahili na Kiha? Wengi wao walijibu kuwa watafitiwa asilimia kubwa kuwa lugha mama yao ni lugha ya Kiha.

Hivyo kufanya mtafiti kugundua kwamba mwalimu anaposhindwa kutoa au kupokea Madhumuni kwa Lugha ya Kiswahili hulazimika kutumia Lugha ya Kiha ili kufikisha taarifa aliyoikusudia au ili wanafunzi waweze kumwelewa Vizuri.

Jedwali Na. 4.2: Idadi ya Watafitiwa Kutomuelewa Mwalimu Wakati wa Kufundishwa Kutokana na Athari ya Kiha

Idadi 5 ya watafitiwa	Ambao hawakusema	Waliokubaliana na hali
30	5	25

4.2.4 Athari katika (Sauti) / Fonolojia

Yule (2010) Matamshi ni utamkaji wa sauti za binadamu kwa kuzingatia muktadha wa mawasiliano ili mawasiliano yaweze kufanyika vizuri yanahitaji utamkaji wa Irabu na herufi vizuri kama inavyotakiwa kutamkwa kulingana na muktadha maalumu. Ni dhahili kuwa wanafunzi wengi wanapojitunza lugha ya pili huweza kufanya makosa makubwa ya kifonolojia. Makosa hayo yanaweza kupoteza maana ya neno husika.

4.2.4.1 Kushindwa Kutamka Baadhi ya Sauti (Ubadilishaji wa Fonimu)

Hapa kutokana na athari ya lugha ya Kiha mtafiti aligundua uwepo wa athari ya kifonolojia iliyotokana na lugha ya Kiha katika ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili. Athari hizo ni kama zifuatazo:-

4.2.4.1.1 Sauti /l/ Kutamkwa Kama Ssauti /r/

Mtafiti aligundua kuwa baadhi ya watafitiwa au watumiaji wa lugha ya Kiha kushindwa kutamka sauli /l/ na kutamka sauti /r/. Pia, aligundua kuwa wanafunzi wanatumia sana sauti /r/ badala ya /l/ kutokana na kuathiriwa kwa lugha yao ya Kiha. Kwa wanaojifunza lugha ya pili, makosa kama haya hutokea sana na huenda yakapungua pale anapoendelea kujifunza lugha ya pili.

Jedwali Na. 4.3:. Sauti /r/ kutamkwa kama Sauti /l/

Neno Sahihi	**Neno lisilo Sahihi**
Lala	Rara
Lakini	Rakini
Lalamika	Raramika
Lia	Ria
Laini	Raini
Lima	Rima

4.2.4.1.2 Sauti/g/ Kutamkwa kama sauti /k/

Jedwali na 4.4 linaonesha athari ya matumizi ya sauti /k/ katika utamkaji wa lugha ya Kiha kama sauti /g/. Mtafiti amegundua kuwa Asilimia kubwa ya watu walioathiriwa na lugha ya Kiha hutumia sauti /g/ badala ya /k/ katika maneno ya Kiswahili. kwa mfano.

Jedwali Na. 4.4: Sauti /g/ Kutamkwa Kama Sauti /k/

Neno Sahihi	Neno lisilo sahihi
Kasulu	Gasuru
Kiazi	Giazi
Kiatu	Giatu
Kisima	Gisima
Kina	Ginu
Karanga	Garanga
Kabati	Gabati

4.2.4.1.3 Sauti /dha/ kutamka kama Sauti /za/

Matokeo ya Utafiti huu yalithibitisha kwamba wanafunzi wa kabila la Kiha hawawezi kutofautisha Sauti /dh/ na (z) za hivyo kutokana na ujifunzaji wa sauti hizi vikwamizi nguna walipata changamoto ya kushindwa kutofautisha sauti hizi kati ya /dh/ na /z/. Mtafiti aligundua changamoto hizi baada ya kuwapa wanafunzi baadhi ya maneno ili kutamka. Maneno hayo ni dharau, dhambi, na dhoruba., .Jedwali 4.5 linaonesha athari ya Sauti /dh/ na sauti /z/.

Jedwali Na. 4.5: sauti /dh/ kutamkwa kama sauti /z/

NENO SAHIHI	NENO LISILO SAHIHI
Dharau	Zarau
Dhambi	Zambi
Dhoruba	Zoruba
Dhihirisha	Zihirisha
Dhabau	Zabau

4.2.5 Athari ya Kimsamiati

Mtafiti aligundua kuwa baadhi ya wanafunzi na watumiaji wa lugha ya Kiha kama lugha mama yao huweza kuchomeka misamiati ya Kiha katika sentensi za Kiswahili kutokana na mwingiliano wa lugha zaidi ya moja katika jamii huweza kusababisha mwingiliano wa misamiati wa lugha moja na lugha nyingine. Kutokana na hoja au swali lililoulizwa kwamba mwingiliano wa lugha moja huweza kusababisha msamiati wa lugha moja kuchopekwa katika lugha nyingine na kujibiwa ndio. Rugatiri_2011 anaeleza kuwa msamiati ni nyanja muhimu katika kuwasiliana. Hivyo, msamiati wa lugha husika ndio ambao hufanya watu kuelewana vizuri. Katika utafiti huu mtafiti amegundua kuwa watumiaji wa lugha ya Kiha huchanganya sana msamiati wa lugha yao katika sentensi za Kiswahili.

Kwa mfano:

Jedwali Na. 4.6: mifano ya athari za kimsamiati 1

Na	Kiha	Kiswahili
1	Ingo	Ingo hapa
2	Mama hayateka Ugali	Mama anateka ugali
3	Yalasishe ejo Mwijolo	Alifika ejo usiku
4	Alaza ejo Mukitondo	Atakuja ejo asubuhi

4.2.6 Athari ya Kimuundo

Pia mtafiti aligundua athari ya kimuundo wa sentensi katika lugha ya Kiswahili ambao umeathiriwa na lugha ya Kiha. Mtafiti amegundua kuwa muundo wa sentensi za Kiha umeathri sana sentensi za Kiswahili kwa kuweka baadhi ya viambishi mwanzo au mwisho wa sentensi lugha ya Kiha. kwa mfano,

Jedwali Na. 4.7: Sentensi za Kiha zinavyoathri muundo wa Sentensi za Kiswahili

Sentensi za Kiha	Sentensi za Kiswahili
Ngo , Ingo	Ngo, anakuja badala ya anakuja
Jewe tekaka	Wewe pikaga –badala ya kusema wewe pika.

4.2.7 Athari ya Kimaana

Mtafiti alibaini kuwa lugha ya Kiha iliathiri lugha ya Kiswahili kimaana ambapo watumiaji wa lugha ya Kiswahili wana tafsiri sisisi na tafsiri ya moja kwa moja. Pia katika lugha ya Kiha kuna tafsiri sisisi ambayo inaathri tafsiri ya moja kwa moja katika lugha ya Kiswahili ambayo huwa ina athari katika lugha ya Kiswahili.

Jedwali Na. 4.8: Linaonesha Mfumo wa Athari za Kimaana / Semantiki

Kiha	**Kiswahili**
Ndamsanzeho Haulizo Tundamsanzeho hauliho	Nimemkata Hayupo Nimemkuta hayupo

Katika mfano huo hapo juu inadhihirisha kuwa wazungumzaji wa Kiha husema Kwamba ndamsanze hauliho akimanisha sijamkuta lakini ukimwambia aseme kwa Kiswahili husema nimemkuta hayupo hivyo hutafsiri maneno haya sisisi ambapo huleta makosa ya kimantiki. Hivyo, hizo ni baadhi ya athari kubwa za lugha ya Kiha katika ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili ambazo zimeonekana ambazo athari hizo zimetokana na athari ya lugha mama na baadhi pia zimetokana na ukosefu wa umilisi wa watu katika lugha ya Kiswahili. Kwa muingiliano huu wa lugha yaani lugha ya Kiha na lugha ya Kiswahili ambao umepelekea lugha ya Kiha kuathiri ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili unajidhihirisha katika vipengele mbalimbali kama ifuatavyo;

a) Mofolojia

Kipengele cha lugha ya mofolojia kina husika katika neno. Hivyo katika lugha ya Kiswahili na lugha ya Kiha mpangilio wa viambishi vinafanana. Yaani, katika maneno ya Kiswahili huwa na mpangilio wa viambishi mfano kiambishi awali huanza katika neno kufuata kiini cha neno ndipo humalizia kiambishi. tamati ingawa kiambishi awali huwa vya aina nyingi kama ifuatavyo.

i) Kiambishi awali cha nafsi

Katika kiambishi hiki awali cha nafsi huweza kuwakilisha nafsi mbalimbali yaani nafsi ya kwanza umoja na uwingi, Nafsi ya pili umoja na uwingi, Pia, nafsi ya tatu umoja na uwingi kiambishi awali cha nafsi huweza kuonesha nafsi mbalimbali kwa mfano:

a) ɑnakuja - ɑ - huwakilisha nafsi ya tatu umoja.
b) Ninakula – Ni – huwakilisha nafsi ya kwanza umoja
c) Mnaimba – huonesha nafsi ya pili uwingi

Hivyo hivyo hata katika lugha ya kiha vipo viambishi vya awali vinavyoonesha nafsi mbalimbali mfano:

a) A-na-kula - Ha-ya-dya
b) Ni-na-imba - Ha-ndi-limba
c) Tu-na-imba - Ha-tu-li-limba

Hivyo ni viambishi vya Kiswahili vinavyojidihirisha katika maneno ya Kiha ambapo hata katika Kiswahili yapo.

ii) Kiambishi awali cha njeo

Hiki ni kiambishi katika maneno kinachowakilisha wakati maalumu ambapo tendo fulani lilitokea au litafanyika katika maneno ya Kiswahili huwa na kiambishi cha njeo ambacho huweza kuonesha wakati ambao tendo maalumu lilitokea au litafanyika na katika

kiambishi cha njeo /wakati huweza kuwakilisha nyakati mbalimbali kama vile wakati ujao, uliopita na wakati uliopo/ sasa.

Mfano wa maneno ya Kiswahili ambavyo yanaviambishi vya njeo ni;

a) Watakuja – ta – huonesha wakati ujao
b) Alikuja - li – huonesha wakati uliopita
c) Anakuja – na – huonesha wakati ulopo wa tendo husika.

Hivyo hivyo, katika lugha ya Kiha vipo viambishi ambavyo huonesha wakati maalumu wa tendo uliofanyika yaani huonesha wakati wa uliopita, ujao, wa sasa au wakati uliopo.

Jedwali Na. 4.9: Mfano wa Viambishi vya Njeo Katika Maneno ya Kha

Kiha	Kiswahili	Kiambishi	Wakati
Ha-ya-teka	A-na-pika	-ya-	Uliopo
Ha-la-teka	A-ta-pika	-La-	Ujao
Ha-la-teke	A-li-pika	-la-	Uliopita
Ha-la-jonga	a-na-lima	-la-	Uliopo
Ya-la-jonze	A-li-lima	-la-	Uliopita

iii) Viambishi Tamati

Viambishi tamati ni viambishi ambavyo vinakaa vya mwisho katika neno, Yaani huyapa maneno maana inayohusika. Viambishi hivyo muda mwingine huitwa viambishi tamati maana, kwa kuwa ndivyo ambavyo huleta maana au humaliza maana ya neno au tendo maalumu. Viambishi hivyo vipo katika maneno ya Kiswahili.

a) Naenda – a – kiambishi tamati, maana
b) Nakuja – a – kiambishi tamati, maana
c) Anasikia – a – kiambishi tamati, maana

Vivyo hivyo katika Lugha ya Kiha ipo Viambishi Tamati katika maneno yao Mfano:

Jedwali Na. 4.10: Viambishi Tamati

Kiha	Kiswahili	Kiambishi	
Gend-a	Naend-a	a	
Nsuk-a	Suk-a	a	
Iluk-a	Kimbi-a	a	
Chez-a	Chez-a	a	
Lil-a	Li-a	a	

Hivyo, vipo viambatanishi tamati maana vingi katika maneno ya Kiswahili ambayo hata katika maneno ya Kiha vipo.

4.3 Sababu Zinazopelekea Lugha ya Kiha Kuathiri Ujifunzaji wa Lugha ya Kiswahili

Katika utafiti huu, mtafiti alibaini kuwa wanafuzni wengi hutumia lugha ya Kiha wawapo madarasani hata katika ujifunzaji asilimia kubwa ya wanafunzi hutumia lugha ya Kiha japokuwa wapo ambao hutumia lugha ya Kiswahili. Pia wapo wanafunzi wengi ambao hutumia lugha ya Kiha katika mawasiliano ya wao kwa wao wawapo madarasani au wanapokuwa maeneo ya ujifunzaji yaani mashuleni kuliko kutumia lugha ya Kiswahili sanifu. Mtafiti amegundua hili kutokana na swali alilouliza wanafunzi lililosema kuwa uwapo shuleni unatumia lugha gani katika mawasiliano? Watafiti wa wanafunzi walio wengi yaani karibia asilimia 99% walijibu kuwa wanatumia lugha ya Kiha wawapo shuleni katika mawasiliano ya wao kwa wao. Sababu hizo ni kama zifuatazo:-

4.3.1 Athari ya Lugha Mama

Katika utafiti huu, mtafiti aligundua kuwa sababu mojawapo iliyopelekea lugha ya Kiha kuathiri ujifunzaji wa lugha ya kiswahili ni athari ya lugha mama. Mtafiti aligundua hili baada ya kuhojiana na watafitiwa yaani wanafunzi, walimu na

wanajamii. watafitiwa hao kwa asilimia 95 walisema kuwa sababu ya lugha ya Kiswahili kuathiriwa na lugha ya Kiha katika ujifunzaji ni kutokana na watoto na watu wengi wanaojifunza lugha ya Kiswahili kuwa Kiswahili ni lugha ya pili na wanakuwa tayari wameshaathiriwa na lugha mama yao ambayo ndio lugha yao ya asili. Hivyo wanafunzi wengi ni wamilisi wa lugha ya Kiha kwa kiwango cha juu ambacho hupelekea kuathri lugha ya Kiswahili katika ujifunzaji mashuleni yaani shule za msingi na sekondari pia. Kutokana na kuwa lugha ya Kiha kuwa lugha ya kwanza, watoto wengi hufahamu lugha ya Kiha kabla ya kufahamu lugha yoyote ile hivyo kupelekea watoto hao wanapojifunza lugha ya Kiswahili kuchanganya maneno, sauti miundo hata maana za maneno ya Kiha katika lugha ya Kiswahili kutokana na athari ya lugha mama zipo athari ndogo ndogo ndani yake ambazo ni;

4.3.1.1 Kuthamini Lugha Mama Zaidi Kuliko Lugha Nyingine

Katika utafiti huu mtafiti ameona sababu nyingine ya lugha ya Kiha kuathiri lugha ya Kiswahili katika ujifunzaji ni pamoja na kuwa watu au watoto wa maeneo haya wanathamini sana lugha ya Kiha zaidi kuliko lugha nyingine yoyote. Hii huonekana ambapo mtu yeyote hawezi kuacha kuongea lugha ya Kiha na kuongea lugha nyingine na endapo akiongea lugha nyingine katika mazungumzo yao ya kila siku huonekana kama mshamba yaani haithamini lugha yale ya asili.

Hivyo, kutokana na kuthamini lugha mama yao ambayo ndio lugha ya Kiha imepelekea ugumu wa kujifunza lugha ya Kiswahili kwa kuwa wanaona kuwa Kiswahili ni lugha ambayo haina thamani kama lugha ya Kiha. Hiyo imepelekea watoto wengi kuthamini sana na kuongea na kuwa umilisi wa lugha ya Kiha kuliko lugha ya Kiswahili na kuona kuwa lugha Kiswahili haina umuhimu wowote kwa

sababu wanaamini kuwa lugha nyingine tofauti na lugha ya Kiha haina thamani kama lugha ya Kiha. Kutokana na hilo inapelekea watoto wengi wanaojifunza Kiswahili katika shule za msingi na sekondari kutoongea Kiswahili fasaha na kujikuta wanapoongea lugha ya Kiswahili kuchanganya na maneno ya lugha ya Kiha kwa kuwa tayari wanaona ina thamani kubwa kuliko lugha nyingine.

4.3.1.2 Ukosefu wa Baadhi ya Sauti Katika Lugha ya Kiha

Data za utafiti huu zinaonesha kuwa ukosefu wa baadhi ya sauti katika lugha ya kiha ndio sababu mojawapo inayopelekea lugha ya kiha kuathiri lugha ya Kiswahili kwa kiwango kikubwa. Hii linaonekana pale ambapo sauti za Kiswahili zipo lakini katika lugha ya kiha haupo kwa mfano sauti /l/ ipo katika lugha ya Kiswahili lakini katika lugha ya kiha haipo. Kuna baadhi ya maneno ya Kiswahili hutumia sauli /l/ kama maneno yafuatayo.

Lima;
Lala;
Lugha;

Hivyo katika lugha ya Kiswahili sauti izo zipo katika maneno balimbali lakini katika lugha ya kiha Sauti /l/ hutamkwa kama sauti /r/ hivyo kupelekea baadhi ya maneno kukosa maana au kupelekea mtu kuelewa maana tofauti na ile iliyokusudiwa na msemaji mfano wa maneno ya Kiswahili yenye sauti /l/ na kutamkwa kama sauti /r/ ni kama yafuatayo.

Jedwali Na. 4.11: Maneno ya Kiswahili Yenye Sauti /l/ na Kutamkwa Kama Sauti /r/

Kiswahili	Kiha
Lala	Rara
Kula	Kura
Lima	Rima
Mila	Mira

Pia zipo sauti tofauti tofauti ambazo katika Kiswahili zipo ila, katika lugha ya kiha hazipo hivyo kupelekea wamilisi au wanaojifunza lugha ya Kiswahili kutumia sauti za kiha ambazo hazitakiwi katika lugha ya Kiswahili au sauti hizo hupelekea kuhalibu neno la Kiswahili au kulifanya neno hilo kukosa maana kamili katika lugha ya Kiswahili. Mfano wa sauti hizo ni kama zifuatazo katika lugha ya Kiha hawana sauti /k/ na badala yake kuweka sauti /g/ kwa kuwa tu katika lugha yao hawana sauti /k/ Mfano: neno Kisima katika lugha ya Kiha wanasema Gisima mfano wa neno katika Lugha ya Kiswahili na Kiha.

Jedwali Na. 12: Katika Lugha ya Kiha Hawana Sauti /k/ na Badala yake Kuweka Sauti /g/ Kwa Kuwa tu Katika Lugha yao Hawana Sauti /k

Neno	kiswahili	Kiha
Kisima	Kisima	Gisima
Kisu	Kisu	Gisu
Kiazi	Kiazi	Giazi
Kiti	Kiti	Giti

4.3.1.3 Malezi

Malezi ya wazazi yanachangia ukuaji wa watoto katika uongeaji wa lugha fulani. Wazazi /walezi wengi katika Jamii ya watu wanaongea lugha ya Kiha huchangia zaidi

katika kuleta athari ya lugha ya Kiha katika ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili katika Shule ya msingi na sekondari kwa kuwa walezi /wazazi hao hutumia muda wote kuwaongelesha watoto wao wakiwa wangali wadogo kwa lugha ya Kiha na kusahau kuwaongelesha lugha tofauti tofauti kama vile Kiswahili na lugha nyingine ili kufanya watoto hao kujifunza lugha na kuwa watumiaji wa lugha tofauti tofauti. Walezi wangewawezesha na kuwaongelesha watoto wao lugha tofauti kama Kiswahili wakiwa bado wadogo wangeweza kuwa wamilisi wa lugha zote mbili yaani lugha ya Kiswahili na lugha ya Kiha. Japokuwa watoto ambao wazazi wao huwaongelesha lugha mbili yaani kiswahil na Kiha. Watoto hao hawajaathriwa sana na lugha ya Kiha katika uongeaji watoto hao hujitahidi sana kuongea vizuri pasipo kuchanganya lugha ya kiha katika lugha ya Kiswahili kifonolojia kisintakisia, kimaana na hata kimofolojia. Hivyo, malezi ni sababu mojawapo ya athari kuwa kubwa kutoka lugha moja hadi lugha nyingine.

Kwa mfano mtoto akilelewa na kuanza kujifunza lugha kwa mara yake ya kwanza akikuta wazazi au walezi wake wanaongea Kiswahili lazima na wao wataongea lugha ambayo walezi/wazazi wao wanaongea na pia kama wakikuta walezi wanaongea lugha tofauti na watoto hufuata lugha ambayo wazazi huongea. Hivyo, watoto huweza kurithi lugha kutokana na wazazi wanatumia lugha gani.

4.3.1.4 Kusahau Baadhi ya Msamiati ya Lugha ya Kiswahili

Jamii ya watu waha au watu wanaoongea lugha ya Kiha wameathriwa sana na lugha yao ya Kiha kusababisha kusahau baadhi ya misamiati ya lugha ya kiswahili hivyo kwa kuwa wanamazoea makubwa ya kuongea lugha ya Kiha muda wote husababisha kuathirika kwa lugha ya Kiswahili kwa kuwa kutokana na uzoefu huo wa kuongea

lugha ya Kiha kwa muda wote hupelekea kusahau baadhi ya msamiati wa lugha ya Kiswahili hiyo hupelekea mtu huyo anapoongea lugha ya Kiha katika sentensi ya Kiswahili. Pia anaweza kuchanganya hata mpangilio wa viambishi vya lugha ya Kiha katika lugha ya Kiswahili Kwa mfano:

Kiswahili –Kiha
Ngo - Nakuja

Sentensi hio imeathiriwa na lugha ya Kiha kwa kuwa sentensi nyingi za lugha ya Kiha huanza na neno ngo ndipo sentensi inaendelea, hivyo mtindo wao huo wa sentensi ya Kiha kutokana na mazoea yao imepelekea hadi kuathiri sentensi ya Kiswahili yaani mazoea hayo yamepelekea hata mtu anapoongea sentensi ya Kiswahili huanza na Ngo. Pia hata katika sentensi za Kiswahili zimepelekea kuchanganya msamiati wa Kiha katika sentensi ya Kiswahili. Kwa mfano;

Nitakuja - ejo

Katika sentensi hiyo badala ya kusema nitakuja kesho anakuwa amesahau msamiati wa Kiswahii ambao ni kesho na kuongea kwa msamiati wa Kiha ejo kwa kumaanisha kuwa atakuja kesho.

4.3.2 Mwingiliano Mdogo wa Makabila Tofauti

Mtafiti amegundua kuwa sababu ya lugha ya Kiha kuathiri lugha ya Kiswahili katika ujifunzaji ni pamoja na mwingiliano mdogo wa lugha tofauti tofauti makabila tofauti mwingiliano wa watu wa makabila tofauti, tofauti katika eneo moja hupelekea watu wa eneo hilo kujitahidi sana kuongea lugha ya kuwa hili kwa sababu kunapokuwa na mwingiliano wa watu wanaoongea lugha mbalimbali, hupelekea watu hao kuongea Kiswahili kwa kuwa kutokana na lugha tofauti tofauti zipo shughuli za kijamii ambazo

zinatakiwa kufanywa kwa pamoja au hata huduma za jamii hapo watu wa makabila mbalimbali hulazimika kuongea lugha ya Kiswahili ili kuweza kushirikiana katika mambo ya kijamii au hata huduma za kijamii mfano, Hospitalini na maeneo mengine tofauti ya kijamii.

Hivyo kutokana na ukosefu mkubwa wa muingiliano wa watu wa Lugha tofauti tofauti umepelekea watu wa sehemu hii kuongea Lugha mama yao tu ambayo ni kiha na kusahau lugha nyingine kama Kiswahili na kutokana na mda wote watoto pamoja na jamii kwa ujumla kuongea lugha ya kiha pekee kupeleka lugha ya Kiswahili kutopewa kipaumbele na ndio sababu ya watu hawa kushindwa kuongea lugha ya Kiswahili kwa ufasaha na pia hio ndio inapelekea kuwepo na ugumu wa ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili wawapo mashuleni kwa kuwa hata wakitoka shuleni huongea lugha ya kiha tu na kusahau Kiswahili.

4.4 Ni Njia Zipi Zitumike Kuondoa Athari ya Lugha ya Kiha Katika Ujifunzaji wa Lugha Ya Kiswahili

Katika utafiti huu inajidhihirisha kabisa kuwa watu wengi wa jamii ya Kiha ikiwa ni wanafunzi walimu na hata wanajamii wameathiriwa sana na lugha ya Kiha kifonolojia, kimofolojia, kisintakisia hata kisemantiki kutokana na athari hizo, waathirika yaani walimu, wanajamii na hata wanafunzi wanatakiwa kutumia njia zifuatazo ili kupunguza athari za lugha ya Kiha katika ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili.

4.4.1 Kuwafundisha Lugha ya Kiswahili Wakiwa Bado na Umri Mdogo

Mtafiti amegundua kuwa kuwafundisha watoto wadogo lugha ya Kiswahili. Yaani Kiswahili iwe kama lugha yao ya kwanza kwa wote wanaoanza kujifunza lugha

itasaidia watoto hao kuwa wamilisi wa lugha ya Kiswahili na kuacha kutumia lugha ya Kiha kama lugha yao ya kwanza katika ujifunzaji wa lugha.

Hii inasaidia watoto wakifundishwa lugha ya Kiswahili wakiwa wangali watoto inawasaidia watoto hawa kuwa wamilisi au wajuzi wa lugha ya Kiswahili. wazazi na walezi wanatakiwa kuhamasishwa kuwapa watoto wao kipaumbele pale wanapojifunza lugha kuanza kuwaongelesha watoto hao kwa lugha ya Kiswahili na kuacha kuwaongelesha lugha asili yaani kiha.

Lugha asili ni lugha inayotokana na wanajamii wa eneo fulani ambao wana mila na desturi na utamaduni ni mmoja (Masanjila na wenzake 2009), hivyo lugha asili ya wanajamii wa Kigoma ni lugha ya Kiha. Jamii hii hutumia sana lugha ya Kiha katika mawasiliano na shughuli zao za kila siku na Asilimia kubwa ya wanajamii wa Kigoma wanatumia lugha ya Kiha katika shughuli zao za kila siku. Hivyo mtafiti anaweza akasema kuwa msingi mzuri wa kuwa mmahili au mjuzi wa lugha fulani ni kujifunza lugha hio tangu utotoni kwa hio ili wanajamii wa Kigoma ili waweze kuwa wamahili wa lugha ya Kiswahili wanatakiwa kujifunza lugha ya Kiswahili tangu wakiwa watoto yaani Kiswahili kuwa lugha ya kwanza na lugha asili yaani Kiha kuwa lugha ya pili.

4.4.2 Kuhimiza Kuongea Lugha ya Kiswahili Wawapo Nyumbani

Katika utafiti huu mtafiti amebaini kuwa watoto wengi wameathiriwa na Lugha ya Kiha kutokana na kuipa kipaumbele lugha ya Kiha kuliko lugha nyingine katika mawasiliano na shughuli nyinginezo wawapo nyumbani. Wanajamii wa Kigoma ambao lugha yao ya asili ni Kiha wameipa sana kipaumbele lugha yao kutokana na kwamba data nyingi zilionesha kuwa watoto wengi wawapo manyumbani katika shughuli zao za kila siku kuongea na hufanya mawasiliano kwa kutumia lugha lugha

ya Kiha tu. Mtafiti amelibaini hili kutoka katika swali lililoko kwenye dodoso lililoulizwa uwapo nyumbani hutumia lugha gani katika kufanya mawasiliano ya kawaida na majibu kwa asilimia 99% wamejibu hutumia lugha ya Kiha kwa muda mwingi imepelekea kuathiriwa lugha ya Kiswahili. Ili kuondoa athari hio wazazi/walezi wanatakiwa kuhimizwa au kusisitizwa kuongea lugha ya Kiswahili katika umri wote yaani wakubwa na watoto pia kuhimizwa kuongea lugha ya kiswahili na pia kufanya mawasiliano ya mara kwa mara wawapo nyumbani kwa kutumia lugha ya Kiswahili na siyo nyingineyo. Wakifanya hivyo wanajamii haowatatumia lugha ya Kiswahili baina yao kwa mawasiliano ya kila siku na itapelekea kuwa wamihili au kukifahamu vizuri Kiswahili baina yao kwa mawasiliano ya kila siku na itapelekea kuwa wamilisi au kukifahamu vizuri Kiswahili na kupunguza athari ya lugha ya Kiha katika ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili katika Shule za msingi na sekondari pia.

4.4.3 Ufundishaji wa Kiswahili Sanifu Mashuleni

Mtafiti amegunndua kuwa ili wanafunzi waache kuchanganya lugha yaani lugha ya Kiha katika lugha ya Kiswahili, walimu lazima wawe wamisili wajuzi wa lugha ya Kiswahili. Walimu lizima wawe na ujuzi au umilisi wa lugha ya Kiswahili wa walimu wa lugha ya Kiswahili wa walimu utasaidia sana wanafunzi kujifunza lugha ya Kiswahili kwa ufasaha zaidi kwa sababu walio wao huongea na pia hufundisha kwa kutumia lugha ya Kiswahili na wakitumia Kiswahili kwa ufasaha zaidi.

Mwalimu asipokuwa mmilisi wa lugha ya Kiswahili huweza kusababisha athari kubwa kutoka lugha moja hadi nyingine na hasa kutoka lugha ya kwanza kuathiri lugha ya pili. Wapo walimu ambao hulazimika kutumia lugha ya Kiswahili ili kuhakikisha wanafunzi wanaelewa mfano mara nyingi huweza kuwaelewesha kwa lugha asili pale

anapokuwa anatangaza jambo fulani kwa wanafunzi ili waweze kuelewa vizuri. Hivyo, walimu wafundishe kwa kutumia lugha ya Kiswahili tena fasaha hili litawasaidia wanafunzi wao kuweza kuongea na kukifahamu vizuri Kiswahili kwa undani zaidi kwa kuwa lugha hio ndio ya kufundishia na walimu wao hufundisha kwa ufasaha zaidi tofauti na mwalimu akifundisha huku anachanganya lugha ya Kiha na Kiswahili atapelekea wanafunzi hao. Kutofahamu kabisa lugha ya Kiswahili au atasababisha lugha ya Kiswahili kuathiriwa zaidi na lugha ya Kiha. Hivyo, walimu wafanye juu chini wafundishe kwa lugha ya Kiswahili tena Kiswahili fasaha na sio vinginevyo.

4.4.4 Kiswahili Kuwa Lugha Rasmi ya Kufundishia Elimu ya Sekondari

Kutokana na lugha ya Kiswahili kuathiriwa sana na lugha ya Kiha, mtafiti ameona kuwa ni vyema Kiswahili kuwa lugha rasmi ya kufundishia yaani katika shule za msingi na hata shule za sekondari. Kiswahili kikiwa lugha rasmi ya kufundishia hasa katika shule za sekondari kitasaidia baadhi ya athari ya lugha ya Kiha katika ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili kupungua kwa kuwa itakuwa lugha ambayo itatumika mara kwa mara na ambayo itatumika kufundishia masomo yote kwa ujumla kasoro somo la kingereza katika shule za sekondari hii itasaidia kufahamu kwa wingi misamiati tofauti tofauti kwa lugha ya Kiswahili. Hivyo ili kuondoa athari ya lugha ya Kiha katika ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili katika shule za msingi Sekondari Kiswahili kuwa lugha rasmi ya kufundishia katika shule za msingi na sekondari kinaweza kupunguza athari kutoka katika lugha ya Kiha.

4.4.5 Matumizi ya Kamusi ya Kiswahili

Pia inaweza kuwa njia nzuri ya kuondoa athari ya lugha ya Kiha katika ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili kamusi za Kiswahili huonesha mambo mengi sana yanavyopaswa

kuwa katika lugha ya Kiswahili kwa mfano katika kamusi ya Kiswahili huonesha jinsi neno linavyotamkwa pamoja na jinsi linavyoandikwa kwa ufasaha zaidi hii husaidia wanaojifunza lugha ya Kiswahili kuweza kujua neno jinsi linavyoandikwa pamoja na maana yake mfano neno lala wengine hutamka kama rara na pia hata katika kuandika watu hushindwa kuandika neno lala vizuri kama inavyotakiwa na badala yake huandika neno rara hivyo kupelekea kupoteza maana iliyokusudiwa na msemaji au muongeaji. Hivyo, kukiwa na matumizi mazuri ya kamusi inaweza kuonesha jinsi neno hilo linavyotakiwa kuandikwa hata kutamkwa pia kwa ufasaha zaidi. Pia matumizi ya Kamusi huweza kuonesha neno na aina yake ya neno kuwa neno hilo ni aina gani ya neno na linaweza kubadilika kuwa aina gani na pia linafanya kazi sehemu gani na pengine kuonesha hadi mfano wake kwa kulifungia mfano wake kwa sentemnsi hata moja. Hivyo, matumizi mazuri ya kamusi ya Kiswahili inaweza kusaidia wanajamii wa Kigoma wanaotumia lugha ya Kiha kama lugha yao asili kupunguza athari tofauti tofauti ambazo zinaathiri lugha ya Kiswahili katika ujifunzaji.

4.4.6 Kiswahili Kitumike Katika Shughuli Za Kijamii Zinazotakiwa Kutumia Lugha ya Kiswahili

Pia ni njia mojawapo ambayo inaweza kusaidia watu wa jamii ya Kigoma kupunguza athari ya lugha ya Kiha katika lugha ya Kiswahili. Zipo baadhi ya sehemu ambazo shughuli za kijamii zinafanyika watu wengi katika shughuli hizo tumia lugha ya Kiha katika mawasiliano sehemu hizo ni kama vile sokoni, mashambani na maeneo hayo kuzungumza au kutumia lugha ya Kiha kunapelekea athari kubwa katika lugha ya Kiswahili. Hivyo, watafiti walijibu kuwa inawezekana katika shughuli nyingi japo sio zote za kiuchumi na kijamii itumike lugha ya Kiswahili katika mawasiliano inaweza ikapelekea wanajamii wa Kigoma, kufahamu vizuri lugha ya Kiswahili na

wakafahamu lugha ya Kiswahili athari itapungua. Hivyo, Kiswahili kikitumika katika baadhi ya shughuli zote za kijamii kama vile, sokoni na hata mashambani, katika taasisi mbalimbali inaweza kusaidia kupunguza athari ya lugha ya Kiha katika ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili katika shule za msingi na sekondari.

4.4.7 Kufanya Semina na Mijadala Mbalimbali ya Lugha ya Kiswahili

Kutokana na jamii ya watu wa Kigoma kuathiriwa sana na lugha ya mama yao ambayo ni Kiha dodoso mbalimbali zilizojibiwa kuhusu njia ya kufaya ili athari ya lugha mama yao kupungua au kuisha kabisa ni pamoja na kuanzisha semina na mijadala mbalimbali ya lugha ya Kiswahili. Mijadala hio itasaidia katika kuhimiza umuhimu wa kuongea lugha ya Taifa yaani Kiswahili pia katika mijadala hio itasisitiza faida za kuongea Kiswahili fasaha. Hivyo, mijadala hio inaweza kusaidia asilimia fulani ya watu wa jamii ya waha kujifunza Kiswahili na pia wale wanaoongea Kiswahili kuweza kuwaelimisha zaidi wenzao kuhusu kuongea lugha ya Kiswahili ambapo itasaidia kupunguza uathirikaji wa lugha ya Kiswahili katika jamii ya Kiha.pia ikiwepo mijadala ambayo itafundisha japo hata kidogo lugha ya Kiswahili itasaidia pia wanajamii wa Kiha kuwa na kuendelea kukifahamu vizuri Kiswahili na baadae kuwa wamilisi wa lugha ya Kiswahili na baadae kuwa wamilisi wa lugha ya Kiswahili na hatimae inaweza kupelekea kuwasaidia watu wengi katika jamii yao matumizi sahihi ya lugha ya Kiswahili kwa ujumla na kupunguza baadhi ya athari zitokanazo na lugha asili katika jamii ya Kiha.

4.4.8 Kutoa Elimu Kuhusu Lugha ya Kiswahili

Watumiaji wengi wa Kiha hutumia lugha ya jamii yao (Kiha) sana kwa kuwa wanaamini lugha mama yao ndio lugha pekee ambayo imepewa kipaumbele na

usipoongea au usipo tumia lugha ya Kiha katika mawasiliano ya kila siku unaonekana kuwa kama unakasumba na kutokana na hilo watoto wengi hulazimika kutumia lugha ya Kiha katika mawasiliano ya kila siku ili waonekane kuwa wanajali na kuheshimu mila na desturi zao. Elimu inabidi itolewe kwa kiasi kikubwa katika jamii ya Kiha kuhusu lugha ya Kiswahili ni ya umuhimu wa lugha ya Kiswahili kwamba ndio lugha rasmi nchini na inatumika katika shughuli zote nchini pia inabidi waelimishwe faida za kufahamu kuongea na kuandika lugha ya Kiswahili. Elimu kwa kiasi cha kutosha kikitolewa na watu wa jamii ya Kiha wakipata na kuelewa elimu hiyo ya lugha ya Kiswahili kuanzia faida hadi umuhimu kwa undani zaidi itasaidia watu wa jamii ya Kiha kujifunza lugha ya Kiswahili kwa undani zaidi ambayo itawasaidia popote waendapo au kupata huduma yoyote mahali popote kwa kutumia lugha ya Kiswahili. Na ujifunzaji wa lugha hiyo ya Kiswahili utasaidia pia kupunguza athari ya lugha ya jamii yao katika ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili.Pia, wakipewa elimu kuhusu lugha ya Kiswahili kuwa ndio lugha rasmi nchini wanaweza kuondoa fikra ya kuwa kiha ndio lugha pekee na kujifunza, lugha ya Kiswahili kwa kuona umuhimu wake katika nchi ambapo itapelekea kupunguza makosa katika ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili.

4.4.9 Kutoa Adhabu Kwa Wanafunzi Wanaoongea Lugha Tofautitofauti Na Lugha Ya Kiswahili Wawapo Shuleni

Hii ni njia pekee ambayo wawapo madarasani au mashuleni kuwahimiza watoto au wanafunzi kuongea lugha ya Kiswahili, mtafiti amelibaini hili baada ya kuuliza swali kwa walimu kuwa ni njia gani mnayotumia ili wanafunzi waweze kuongea lugha ya Kiswahili wawapo katika mazingira ya shuleni na walimu hao walijibu kuwa wale waliongea lugha ya jamii husika yaani Kiha waliwapa adhabu na mfano wa adhabu hio ni pamoja na kuvishwa kidani chenye kimewekewa konokono.

Walimu waliendelea kusema kuwa kutokana na adhabu tunazowapa watoto au wanafunzi wanaongea lugha ya jamii yao inasaidia sana kuwafanya wanafunzi hao kuongea lugha ya Kiswahili muda wote wawapo maeneo ya shule kutokana na kuogopa adhabu ya kuvishwa kwa kidani chenye konokono. Hivyo, adhabu hizo ndogondogo zinasaidia wanafunzi kuongea lugha ya Kiswahili wawapo mazingira ya shuleni ambayo pia husaidia baadaye kukifahamu vizuri Kiswahili au hata kufahamu lugha ya Kiswahili na lugha mama yao (Kiha) hivyo itasaidia na inasaidia kupunguza athari ya lugha ya Kiha katika ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili katika shule za msingi na sekondari.

SURA YA TANO

MUHTASARI, MAPENDEKEZO NA HITIMISHO

5.1 Utangulizi

Hii ni sura ya mwisho katika utafiti unaohusu athari ya lugha ya Kiha katika ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili katika shule za msingi na sekondari wilayani Kasulu. Sehemu hii inaelezea utafiti huu kwa ujumla pia, unaelezea matokeo yote yaliyotokana na utafiti huu, mchango wa mtafiti katika jamii husika kwa wanajamii wa kufanyiwa utafiti na baada ya hayo sehemu hii pia itaonesha mapendekezo kutoka kwa mtafiti na watafiti juu ya athari ya lugha ya Kiswahili chanzo cha athari hizo ni lugha ya Kiha kutokea pamoja na njia za kutumia ili kupunguza athari za lugha ya Kiha katika ujifunzaji wa lugha Kiswahili kwa ujumla. Pia, unaonesha maeneo yatakayo hitajika kufanyiwa utafiti tena au kwa undani zaidi.

5.2 Muhtasari wa Utafiti Huu

Mtafiti alitafiti juu ya athari ya lugha ya Kiha katika ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili katika shule za msingi na sekondari wilayani Kasulu. Utafiti huu ulifanyika katika wilaya ya Kasulu mkoa wa kigoma, utafiti huu uliwahusisha wanajamii wa Kigoma ambao lugha yao mama ni Kiha, ambapo utafiti huu ulihusisha watafitiwa 45 walioshiriki kikamilifu katika kutoa taarifa zilizohitajika na mtafiti. Kati ya watafitiwa hao 45, watafitiwa 20 walikuwa ni wanafunzi wa sekondari na shule ya msingi. Watafiti wa 10 walikuwa ni walimu wa shule ya msingi na sekondari. Watafitiwa 15 walikuwa ni wanajamii wanaofahamu lugha ya Kiswahili na lugha ya Kiha.

Lengo kuu la utafiti huu ni kuchunguza athari ya lugha ya Kiswahili katika shule za msingi na sekondari wilayani Kasulu. Malengo mahususi yalikuwa; kubainisha athari

ya lugha ya Kiha katika kazi za ujifunzaji wa lugha ya Kiha katika shule za msingi na sekondari wilayani Kasulu. Pili, ni kubaini sababu mbalimbali zinazopelekea lugha ya Kiha kuathiri lugha ya Kiswahili na lengo la mwisho likiwa ni kutafuta njia za kutatua athari hizo zinazopelekea lugha ya Kiha kuathiri lugha ya Kiswahili. Katika utafiti huu ulichanganya jinsia ya watafiti yaani kulikuwa watafiti wanawake kwa wanaume. Pia, ngazi za elimu za watafiti wa zilichanganywa. Mbinu zilizotumika za kukusanya takwimu katika utafiti huu ni hojaji, majadiliano pamoja na mahojiano, mbinu hizi zote zilimsaidia mtafiti kupata majibu sahihi na takwimu zilizotakiwa kutoka kwa watafiti ingawa kila mbinu ilitumika kwa sampuli zote za watafiti wa taarifa katika utafiti huu zilichanganuliwa kwa njia ya taarifa na maelezo.

Utafiti huu uliongozwa na dhana ya mawasiliano ambayo iliasisiwa na (Giles 1973) ambayo inahusu ulinganisho wa lugha au mawasiliano. Na lengo kuu la utafiti huu ikiwa ni kuchunguza athari za lugha ya Kiha katika ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili katika shule za msingi na sekondari wilayani Kasulu. taarifa hizo zilipatikana katika utafiti huu zimeanishwa na kuchambuliwa vizuri katika sura ya nne kama zinavyotakiwa.

5.3 Matokeo ya Utafiti

5.3.1 Athari ya Lugha ya Kiha katika Ujifunzaji wa Lugha ya Kiswahili katika Shule za Msingi na Sekondari

Kutokana na utafiti huu, mtafiti alibaini kuwa kuna athari kubwa ya lugha ya Kiha katika lugha ya Kiswahili ambazo athari hizo zinaathiri lugha ya Kiswahili kifonolojia, mofolojia, sintaksia, pamoja na kisemantiki. Athali hizo ni kama Kutamka /g/ badala ya /k/, kutamka r/ badala ya /l/, Kutamka /bha/ badala ya /b/, kutamka /z/ badala ya

/dh/. Kupachicha viambishi mbele ya msamiati ambavyo havitakiwi kupachika baadhi ya viambishi ambavyo havihusiki kabla ya neno; kuchanganya msamiati wa lugha ya Kiha katika sentensi za Kiswahili. Kuchanganya muundo wa sentensi za Kiha na muundo wa sentensi za Kiswahili.

5.2.2 Kubainisha sababu za Lugha ya Kiha kuathiri Lugha ya Kiswahili katika Ujifunzaji katika Shule za Msingi na Sekondari

Zipo sababu kuu moja iliyo sababisha lugha ya kiha kuathiri lugha ya Kiswahili ambapo ndani yake kuna sababu ndogo ndogo sababu hizo ni;

Athari ya lugha mama, hii ndio sababu kubwa aliogundua mtafiti iliyopelekea lugha ya Kiswahili kuathiriwa na lugha ya kiha. Katika lugha nyanja zote na nyingine ni ndogo ndogo ndani ya athari ya lugha mama ambazo ni; Kuthamini lugha mama kuliko lugha nyingine, malezi, kusahau baadhi ya misamiati ya lugha ya Kiswahili ukosefu wa baadhi ya sauti katika lugha ya Kiha na muingiliano mdogo wa makabila tofauti

5.2.3 Kubaini njia za kutumia ili kupunguza athari za Lugha ya Kiha katika Ujifunzaji wa Lugha ya Kiswahili katika Shule za Msingi na Sekondari

Hizi ni njia ambazo zitasaidia kupunguza athari ya lugha ya Kiha katika lugha ya Kiswahili ambazo zimependekezwa kutumika na wanajamii wa Kiha ili kupunguza au kuondoa athari ya Kiha katika ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili njia hizo ni kama.

Kuwafundisha watoto lugha ya Kiswahili wakiwa na umri mdogo, kuhimiza kuongea lugha ya Kiswahili wawapo nyumbani, ufundishaji wa Kiswahili sanifu wawapo shuleni, Kiswahili kuwa lugha ramsi ya kufundishia, matumizi ya kamusi ya Kiswahili, Kiswahili kitumike katika shughuli zote za kijamii, kufanya semina na mijadala mbalimbali ya lugha ya Kiswahili, kutoa elimu kuhusu lugha ya Kiswahili na kutoa adhabu kwa wanafunzi waoongea lugha tofauti na Kiswahili.

5.3 Mchango wa Utafiti

Matokeo ya utafiti huu yana mchango mkubwa katika taasisi, elimu, serikali na hata jamii kwa ujumla ambayo matokeo ya utafiti huu yataleta musukumo ukuaji wa lugha ya Kiswahili kutokana na kubainika kwa mbinu ambazo zitasaidia kupunguza athari ya lugha ya Kiha katika lugha ya Kiswahili ambapo itasaidia kukua kwa lugha ya Kiswahili sanifu endapo njia hizo za kupunguza athari zitatumika ipasavyo. Pia, utafiti huu unamchango kwa kuwa unaweza kutumika kwa kurejerewa na wasomi wengine wanaofanya tafiti lugha mama zingine, au lugha kwa ujumla, pia utafiti huu utasaidia sana watu kupitia njia za kupunguza athari zinazoathiri lugha ya Kiswahili katika ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili kwa ujumla.

5.4 Mapendekezo ya Utafiti

Kutokana na takwimu alizozipata mtafiti, kuhusu athari ya lugha ya Kiha katika kujifunza lugha ya Kiswahili, mtafiti anapendekeza kuwa walimu, wawapo darasani wajitahidi sana kutumia lugha ya Kiswahili fasaha wanapokua wanafundisha na sio tu darasani hata katika mazingira yote ya shuleni yaani nje na ndani ya darasa, hii itasaidia wanafunzi nao kutumia Kiswahili fasaha wawapo mazingira yote ya shuleni katika kufanya mazungumzo kwa muda wote.

Pia, mashirika mbalimbali yanayohusiana na ukuaji na uendeshaji na utumiaji wa lugha ya Kiswahili kama vile Baraza la Kiswahili Tanzania (BAKITA) na vyombo vya habari kuhamasisha matumizi ya lugha ya Kiswahili kila wakati na pia kuweka vipindi mbalimbali katika vyombo vya habari vitakavyohamasisha na kutoa elimu juu ya lugha ya Kiswahili na kuhamasisha kutumia lugha ya Kiswahili sanifu muda wote hili itasaidia watu kuongea na kukipenda Kiswahili. Vilevile, wazazi wajitahidi sana

kuhimiza watoto na kuelimisha juu ya umuhimu wa lugha ya Kiswahili na kuwasistiza faida ya kutumia Kiswahili sanifu

5.5 Mapendekezo ya Tafiti zijazo

Mtafiti alietafiti kuhusu athari ya lugha ya kiha katika ufunzaji wa lugha wa lugha ya Kiswahili ninapendekeza kuwa lugha ya kiha haijafanyiwa tafiti za kutosha na kwa kina zaidi kuhusiana na ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili kwa kuwa utafiti huu umeshughulikia athari ya lugha ya kiha katika ufunzaji wa lugha ya Kiswahili, katika shule za msingi na sekondari wilayani kasulu, Ninapendekeza kufanyike tafiti zinginezo zitakazo husu athari ya lugha ya kiha katika kizungumza lugha ya Kiswahili kwa ujumla.

Pia, napendekeza watafiti wajao kuweza kutafiti sababu moja na kuchukua kama kichwa cha utafiti na kukichunguza kwa ndani zaidi na kupata taarifa za ndani zaidi. Kwa kuwa inawezekana athari moja ya lugha ya kiha kufanyiwa utafiti zaidi kwa mfano angetokea mtafiti akatifiti juu ya lugha mama jinsi inavyopelekwa Kiswahili kuathiriwa kifonolojia, mofonolojia na hata kisintakisia.

5.6 Hitimisho

Kupitia utafiti huu mtafiti ameweza kugundua athari za lugha ya Kiha katika ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili katika shule za msingi na sekondari na athari hizo zikiwa ni mchanganyiko wa athari za kifonolojia, mofolojia, sintaksia pamoja na athari za kisemantiki katika lugha ya Kiswahili. Wanafunzi wa Kiha wameathiriwa sana na lugha yao ya Kiha kwani imebainika kuwa wanafunzi hao hutumia lugha ya Kiha wawapo madarasani katika mazungumzo ya wao kwa wao, Pia, hutumia lugha ya kiha katika shughuli zote za kijamii wawapo nyumbani hutumia lugha ya Kiha katika

kuwasiliana wao kwa wao pamoja na wao wakiwa wanawasiliana na wazazi wao. Hivyo, kutokana na hilo inatakiwa watu na mashirika mbalimbali kwa pamoja kutoa elimu katika jamii hii kuhusiana na utumiaji wa lugha ya Kiswahili ili kuweza kupunguza athari hizo pia mjadala na kongamano pamoja na vipindi vinavyofundisha lugha ya Kiswahili katika redio, shuleni na hata nyumbani.

Hivyo, ili tatizo hili liweze kupungua katika shule, ni vizuri kuanzisha vikundi vya kujifunza na kuongea Kiswahili sanifu mashuleni na kuweka midahalo inayosaidia wanafunzi kuwajengea uwezo wa kuongea Kiswahili sanifu mbele ya wenzake nje na ndani ya mazingira ya shuleni. Pia, walimu watumie Kiswahili sanifu wanapofundisha na wanapofanya mawasiliano wakati wote wawapo shuleni itapelekea wanafunzi kuiga mazungumzo ya walimu wao ambao itasaidia wanafunzi hao kuanza kujifunza lugha ya Kiswahili taratibu taratibu na baadaye kuwa wamilisi wa lugha ya Kiswahili.

MAREJEREO

Cook, R., Rodman, R., & Hyms, N. (1969). *An introduction to language* (8th ed.). Boston, MA: Thomson Wadsworth.

Cooper, (1989). *Research method techniques and procedures*. London: University Press.

Corder, S. P. (1967). *Error analysis and interlanguage*. Oxford: Oxford University Press.

Crystal, D. (2008). *Texting: The gr8 db8*. Oxford: Oxford University Press.

Curtain, E. (1990). *The impact of Bantu language on English language learning process in Tanzanian secondary schools*.

Enon, C. J. (1995). *Education research, statistics, and measurement*. Kampala: Makerere University Press.

Ghanen. (2005). The child between two languages. In M. Kara (Ed.), *Second language acquisition: Learners' errors and error correction in language teaching* (pp. xx–xx).

Giles, H. (1973). Ethnicity markers in speech. In K. R. Scherer & H. Giles (Eds.), *Social markers in speech* (pp. xx–xx). London: Cambridge University Press.

Habwe, & Kalanje, P. (2004). *Misingi ya sarufi ya Kiswahili*. Nairobi: Phoenix Publishers.

Kihore, Y. M. (2003). *Sarufi maumbo ya Kiswahili sanifu (Mamlaka) sekondari na vyuo*. Dar es Salaam: Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili (TUKI).

Kisakwah, B. A. (2014). *Uchunguzi wa makosa na muundo wa sentensi: Ulinganisho wa sentensi sahili za Kiswahili sanifu na za Kisuba* (Tasinifu ya Udhamili). Chuo Kikuu cha Nairobi.

Kombo, D. K., & Tromp, D. L. A. (2006). *Proposal and thesis writing: An introduction*. Nairobi: Paulines Publications Africa.

Kothari, R. C. (1990). *Research methodology: Methods and techniques*. New Delhi: New Age International.

Kothari, R. C. (2008). *Research methodology: Methods*. New Delhi: New Age International.

Kothari, R. C. (2014). *Research methodology: Methods and techniques* (3rd ed.). New Delhi: New Age International.

Kothari, R. C. (2014). *Research methodology: Techniques*. New Delhi: New Age International.

Masanjila, Y. P. (2009). *Isimu jamii: Sekondari na vyuo*. Dar es Salaam: Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili (TUKI).

Masasa, M. A. (2017). *Athari ya matamshi ya lugha ya Kijita katika kujifunza lugha ya Kiswahili*.

Masebo, J. A., & Nyangwine, N. (2008). *Nadharia ya lugha: Kiswahili kidato cha tano*. Dar es Salaam: Nyambari Nyangwine Publishers.

Massamba, D. P. B. (2004). *Kamusi ya isimu na falsafa ya lugha*. Dar es Salaam: TUKI.

Massanjila, Y. P., et al. (2009). *Isimu jamii*. Dar es Salaam: TUKI.

Mekacha, R. D. H. (2000). *Nadharia ya muktadha wa Kiswahili*. Osaka: Osaka University of Foreign Studies.

Mekacha, R. D. K. (2000). *Isimu jamii: Nadharia na muktadha wa Kiswahili*. Osaka: Osaka University of Foreign Studies.

Otiende, M. A. (2013). *Athari ya mofolojia ya Kibasuba katika matumizi ya Kiswahili kama lugha ya pili* (Tasnifu ya MA).

Rocha. (2011). *Kiswahili: Past, present and future horizons*. Nairobi: University Press.

Selinker, L. (1969). *Language transfer: General linguistics*. New York: Row, Peterson.

Singh, K. (2007). *Quantitative social research methods*. New Delhi: SAGE Publications.

Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili. (2004). *Kamusi ya Kiswahili sanifu*. Dar es Salaam: Oxford University Press.

TUKI. (2004). *Kamusi ya Kiswahili sanifu*. Nairobi: Oxford University Press, East Africa Ltd.

Walliman, N. (2011). *Research methods: The basics*. London & New York: Routledge Taylor & Francis Group.

Yule, G. (2010). *The study of language*. Cambridge: Cambridge University Press.

MASWALI YA HOJAJI KWA WATAFITIWA

Maswali kwa Wanafunzi

Mimi ni RUKIA MSAGO JUMA ninasoma wa shahada ya pili (Uzamili) kwamasomo ya Isimu ya Lugha katika chuo Kikuu Huria cha Tanzania. Ninafanya utafiti juu ya athari ya lKiha katika ujifunzaji wa Lugha ya Kiswahili huu ni utafiti ambao utanisaidia kukamilisha Shahada yangu ya Uzamili. Naomba ushirikiano katika kunisaidia kujibu maswali hapo chini.

Kidato ………………………………………..
Jinsia …………………………………………..

1. Je unafahamu vizuri lugha ya Kiha?
   a) Ndio
   b) Hapana

2. Je unaifahamu vizuri Lugha ya Kiswahili?
   a) Ndio
   b) Hapana

3. Uwapo Shuleni unatumia Lugha gani katika mawasiliano?
   a) Kiswahili
   b) Kiha

4. Uwapo Nyumbani na katika shughuli ndogo ndogo hutumia Lugha gani katika kuwasiliana?
   a) Kiha
   b) Kiswahili

5. Je kati ya Kiswahili na Kiha ipi ni Lugha yako ya kwanza? ……………………………..

6. Je ni dhahiri kuwa Kiha kimeathiri Lugha ya Kiswahili. Kimsamiati,Kimaana, Kimuundo na Kisauti?
   a) Ndio

b) Hapana

Kama jibu ni Ndio taja maneno matatu ya Kiha ambayo pia yanatumika katika Kiswahili.

i) ______________________________________

ii) ______________________________________

iii) ______________________________________

7. Orodhesha athari hasi na athari chanya ya lugha ya Kiha katika kujifunza Lugha ya Kiswahili.

(i) Athari chanya

____

____

____

(ii) Athari hasi

____

____

____

8. Taja sababu 4 zinazopelekea Lugha ya Kiha kuathiri Lugha ya Kiswahili

____

____

____

9. Unafikili tunaweza kufanya nini ili kuondoa athari hizo za Kiswahili

i) _______________________________

ii) _______________________________

Hojaji kwa Walimu wa Shule za Msingi na Sekondari wanaofundisha Kiswahili

Mimi RUKIA MSAGO JUMA ninasomawa shahada ya pili (Uzamili) kwamasomo ya Isimu ya Lugha katika chuo Kikuu Huria cha Tanzania. Ninafanya utafiti juu ya athari ya lugha ya Kiha katika ujifunzaji wa Lugha ya Kiswahili huu ni utafiti ambao utanisaidia kukamilisha Shahada yangu ya Uzamili. Naomba ushirikiano katika kunisaidia kujibu maswali hapo chini.

- Umri
- Kiwango cha Elimu

Chagua herufi ya jibu sahihi

1. Je ni kweli kuwa Lugha ya Kiha inaathiriana na Lugha ya Kiswahili Kimatamshi, Kimsamiati, Kisauti na hata Kimuundo.
   a) Ndio
   b) Hapana

Kama jibu lako ni ndio toa mifano ya athari hizo za Kiha katika kujifunzaKiswahili.

- Athari ya Kisauti / Fonology

  ____
  ____
  ____

- Athari ya Kimatamshi

  ____
  ____
  ____

- Athari ya Kimaana

  ____
  ____
  ____

- Athari za kimuundo

  ____
  ____
  ____

2. Taja sababu 5 zinazosababisha Kiswahili kuathiriwa na Kiha.
   i) ____
   ii) ____
   iii) ____
   iv) ____
   v) ____

3. Ni kipi kifanyike ili kuondoa athari za Kiha katika ujifunzaji wa Kiswahili.

   ____
   ____

4. Je unafahamu Kiha vizuri na kiswahili vizuri
   a) Ndio
   b) Hapana

5. Je mnatumia njia gani kuhakikisha kuwa wanafunzi wanaongea Kiswahili Fasaha.
   i) ______________________________
   ii) ______________________________
   iii) ______________________________

6. Wanafunzi wanapokuwa Darasani wanazungumza kwa kutumia Lugha gani
   (a) Kiha
   (b) Kiswahili
   (c) Zote mbili

7. Mkiuliza Swali darasani wanafunzi hutumia lugha gani kujibu
   a) Kiswahili
   b) Kiha
   c) Zote mbili

8. Unapokuwa darasani unatumia Lugha gani kuwaelewesha wanafunzi ili waelewe?
   ____

9. Njia zipi zifanyike ili kuondoa athari ya Kiha katika ujifunzaji wa Kiswahili
   ____
   ____
   ____

Hojaji kwa wanajamii

Mimi RUKIA MSAGO JUMA ninasomawa shahada ya pili (Uzamili) kwamasomo ya Isimu ya Lugha katika chuo Kikuu Huria cha Tanzania. Ninafanya utafiti juu ya athari ya Kiha katika ujifunzaji wa Kiswahili huu ni utafiti ambao utanisaidia kukamilisha Shahada yangu ya Uzamili. Naomba ushirikiano katika kunisaidia kujibu maswali hapo chini.

1. Ni lugha gani ambayo huwa inatumika katika mawasiliano mkiwa nyumbani
   a) Kiswahili
   b) Kiha

   Kama ni Kiswahili toa sababu na kama ni Kiha toa sababu.
   ____
   ____
   ____
   ____

2. Kiswahili ni Lugha ya Kwanza au ya Pili kwako? ____________________

3. Ni kwa nini Wanafunzi wameathiriwa na Kiha katika kujifunza Kiswahili.

2. ____
____
____

4. Ni njia zipi zinazoweza kupunguza athari hizo kwa wanafunzi au wale wote wanaojifunza Kiswahili na Kiha ndio Lugha yao ya Kwanza.

   ____
   ____
   ____
   ____

5. Taja misamiati mitano ambayo inaonesha athari ya Kiha katika kujifunza Kiswahili
   i) ________________________________
   ii) ________________________________
   iii) ________________________________

iv) ______________________________
v) ______________________________

6. Taja athari mbalimbali za Kiha zinazoathiri Lugha ya Kiswahili

____
____
____
____
____
____
____
____
____

7. Je watoto wakiwa Nyumbani hutumia l Kiswahili katika mawasiliano?
   a) Ndio
   b) Hapana

8. Taja maneno ya Kiha yanayoathiri vipengele katika Kiswahili.
   i) __________________________________
   ii) __________________________________
   iii) __________________________________
   iv) __________________________________
   v) __________________________________

9. Je matumizi ya Lugha mbili kwa wakati mmoja unaweza sababisha Lugha moja kuathiri Lugha nyingine.
   a) Ndio
   b) Hapana

10. Je wanafunzi wanapokuwa nyumbani hutumia Lugha gani katika Mawasiliano baina yao na wazazi
   (a) Kiswahili
   (b) Kiha

MAHOJIANO

Maswali ya mahojiano baina ya mtafiti na watafitiwa na maswali haya yatatumika kwa alengwa wote kwa wakati na makundi tofauti tofauti yaani maswali haya yatatumika kwa walimu, wanafunzi, na wazazi au wanajamii lengwa.

Kuhoji maswali kadri uwezavyo.

i) Mnafahamu kuongea Lugha ya Kiha
(a) Ndio (b) Hapana

ii) Unafahamu Kiswahili?

iii) Katika mawasiliano ya kila siku hutumialugha gani hasa? Kiswahii au kiha ? kwa nini?

iv) Taja athari ya lugha ya kiha katika lugha ya Kiswahili
________________________________,
________________________________,
________________________________,

v) Taja maneno matano ya Kiswahili yaliyoathiriwa na lugha ya Kiha
_________________________________,
_________________________________,
_________________________________,
_____________________________________,
______________________________________,

vi) Unaweza nitajia maneno matano yanayoingiliana kati ya Kiha na Kiswahili?
____
____
____
____
____

vii) Je njia zipi zinazoweza kuondoa athari hizo za Lugha ya Kiha katika Kiswahili?

viii) Je athari hizo zinaweza kupungua endapo tukifanya nini?
_________________________________,
_________________________________,
_________________________________,

ix) Ni sababu zipi zinazopelekea athari hizo kutokea?
____
____
____

MAJADILIANO

Maswali ya majadiliano baina ya mtafiti na watafitiwa na maswali haya yatatumika kwa alengwa wote kwa wakati na makundi tofauti tofauti yaani maswali haya yatatumika kwa walimu, wanafunzi, na wazazi au wanajamii lengwa.

Kuhoji maswali kadri uwezavyo.

i) Mnafahamu kuongea Lugha ya Kiha
   (a) Ndio (b) Hapana

ii) Unafahamu Kiswahili?

iii) Katika mawasiliano ya kila siku hutumialugha gani hasa? Kiswahii au kiha ? kwa nini?

iv) Taja athari ya l kiha katika Kiswahili

______________________________,
______________________________,
______________________________,

v) Taja maneno matano ya Kiswahili yaliyoathiriwa na Kiha

_______________________________,
_______________________________,
_______________________________,
___________________________________,
____________________________________,

vi) Unaweza nitajia maneno matano yanayoingiliana kati ya Kiha na Kiswahili?

____
____
____
____
____

vii) Je njia zipi zinazoweza kuondoa athari hizo za Kiha katika Kiswahili?

viii) Je athari hizo zinaweza kupungua endapo tukifanya nini?

_______________________________,
_______________________________,
_______________________________,

ix) Ni sababu zipi zinazopelekea athari hizo kutokea?

____
____

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

MINISTRY OF EDUCATION, SCIENCE AND TECHNOLOGY

THE OPEN UNIVERSITY OF TANZANIA

Ref. No OUT/ PG201901191 **24th January, 2023**

Regional Administrative
Secretary, Kigoma Region,
P.O Box 125,
KIGOMA.

Dear Regional Administrative Secretary,

RE: RESEARCH CLEARANCE FOR MS RUKIA MSAGO JUMA, REG NO: PG201901191

3. The Open University of Tanzania was established by an Act of Parliament No. 17 of 1992, which became operational on the 1st March 1993 by public notice No.55 in the official Gazette. The Act was however replaced by the Open University of Tanzania Charter of 2005, which became operational on 1st January 2007.In line with the Charter, the Open University of Tanzania mission is to generate and apply knowledge through research.

4. To facilitate and to simplify research process therefore, the act empowers the Vice Chancellor of the Open University of Tanzania to issue research clearance, on behalf of the Government of Tanzania and Tanzania Commission for Science and Technology, to both its staff and students who are doing research in Tanzania. With this brief background, the purpose of this letter is to introduce to you **Ms. Rukia Msago Juma, Reg. No: PG201901191)** pursuing **Master of Arts in Kiswahili**

(MA-KISWAHILI). We here by grant this clearance to conduct a research titled **“Athari ya Lugha ya Kiha katika Ujifunzaji wa Lugha ya Kiswahili katika Shule za Msingi na Sekondari Wilayani Kasulu”.** She will collect her data at Kasulu District in Kigoma Region from 25th January to 25th February 2023.

5. In case you need any further information, kindly do not hesitate to contact the Deputy Vice Chancellor (Academic) of the Open University of Tanzania, P.O.Box 23409, Dar es Salaam. Tel: 022-2-2668820.We lastly thank you in advance for your assumed cooperation and facilitation of this research academic activity.

Yours sincerely,

THE OPEN UNIVERSITY OF TANZANIA

Prof. Magreth S.Bushesha

For: VICE CHANCELLOR

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

Anuani ya simu: "MKUUWAMKOA "
Simu Na: 028-2802287/2330
Nukushi: 028-2802330
Barua pepe: ras@kigoma.go.tz

Ofisi ya Mkuu wa Mkoa,
Mkoa wa Kigoma,
2 Mtaa wa Mkoani,
S.L.P. 125,
47180 KIGOMA.

Unapojibu tafadhali taja:

Kumb.Na.DA.73/274/02"N"/242

08 Machi, 2023

Mkurugenzi Mtendaji,
Halmashuri ya Wilaya Kasulu,
S.L.P 97,
KASULU.

YAH: **KIBALI CHA KUFANYA UTAFITI KUHUSU ATHARI YA LUGHA YA KIHA KATIKA UJIFUNZAJI WA LUGHA YA KISWAHILI KATIKA SHULE ZA MSINGI NA SEKONDARI WILAYANI KASULU**

Tafadhali husika na mada tajwa hapo juu.

2. Ofisi imepokea barua kutoka Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye Kumb.Na.AB.307/323/01 ya tarehe 02 Machi, 2023 kuhusu mada tajwa hapo juu.

3. Ofisi ya Rais – TAMISEMI imetoa kibali kwa **Bi. Rukia Msago Juma**, Mwanafunzi kutoka Chuo Kikuu Huria cha Tanzania (OUT) kwa ajili ya kufanya utafiti tajwa katika Halmashauri ya Wilaya Kasulu.

4. Muda wa kufanya utafiti huu ni kati ya tarehe 28 Februari, 2023 na tarehe 28 Machi, 2023. Ofisi ya Rais – TAMISEMI kwa kushirikiana na Taasisi nyingine za Serikali itafanya ukaguzi wakati wowote kujiridhisha na utekelezaji sahihi wa kibali hiki. Takwimu zitakazokusanywa kutokana na utafiti huu ni kwa ajili ya matumizi ya ndani tu na iwapo zitatakiwa kuchapishwa na kusambazwa kibali kutoka Mamlaka husika kitapaswa kuombwa.

5. Kwa barua hii, unaelekezwa kutoa ushirikiano utakaohitajika na kukamilisha utafiti huu kama ilivyokusudiwa. Kazi hii isimamiwe na Mtakwimu wa Halmashauri husika na kutoa taarifa ya utekelezaji.

6. Ninashukuru kwa ushirikiano.

Albert G. Msovela.
KATIBU TAWALA WA MKOA
KIGOMA.

Nakala: Katibu Mkuu,
OR – TAMISEMI,
S.L.P.1923,
DODOMA.

KATIBU TAWALA WA MKOA
KIGOMA